# **UWT** yatangaza itamkana Gekul, kashfa ikithibitika

UKURASA 2



# **Mtoto** achomwa mikono madai ya kudokoa mboga

UKURASA 3



## YANGA: AL AHLY WAMESHIKILIA HESHIMA YETU

UKURASA 24


# Nipashe

Jumatano Novemba 29, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581509

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Ukweli uongozi mpya CCM leo

UKURASA 2



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo



Abdallah Bulembo



Dk. Emmanuel Nchimbi



Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan

# MOI yapoteza Mil. 300/- kila mwezi kisa msamaha

UKURASA 4



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Mathew Kundo, akionyesha ripoti ya utafiti wa hali ya unyanyasaji wa kijinsia kwenye vyombo vya habari, baada ya kuizindua katika Maadhimisho ya 36 ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa TAMWA, Rose Reuben, (nyuma kushoto) ni Mkurugenzi wa Klabu za Waandishi wa Habari nchini (UTPC), Kenneth Simbaya na viongozi wengine wa chama hicho. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 3

## MFUKO UWEKEZAJI KUCHOCHEA UKUAJI MASHIRIKA YA UMMA

OFISI ya Msajili imeanza utekelezaji wa kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ambao utasaidia kimtaji...

UKURASA WA 5

## MKENDA: UBORA WA VYUO VIKUU AFRIKA UIMARISHWE

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amewataka...

# TAMWA yanyoosha kidole kwa wahariri, mameneja ukatili vyombo vya habari

UKURASA 4

**MICHEZO** BENCHIKHA AONYA MASTAA SIMBA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI), Prof. Abel Makubi (kushoto), kabla ya kuzindua miradi mbalimbali ya utoaji huduma hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukweli uongozi mpya CCM leo

**Na Mwandishi Wetu**

KIKAO cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinafanyika leo jijini Dar es Salaam, hisia zote za umma zikiangukia uamuzi na uteuzi wa Katibu Mkuu wa chama.

Mjumuiko huo wa vigogo wa chama hicho, unachukua nafasi, ajenda kuu ya hadhira inayotega masikio na hisia ni majibu ya tetesi zilizotawala kuhusu kujiuzulu kwa Katibu Mkuu Daniel Chongolo.

Ni tetesi zenye ushahidi usiothibitishwa mitaani kupitia mitandao ya kijamii, kujiuzulu kwa Chongolo kwa sababu zilizotajwa kwenye barua iliyooneshwa mitandaoni, kwamba 'anakabiliwa na kashfa'.

Mawasiliano hayo ya kwenye mitandao ya kijamii, yakasambaza tetesi za mbadala wake, zikitaja majina ya vigogo wakiwamo Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, Mzee John Chiligati na Abdallah Bulembo.

Hayo yanatokea ilhali Chongolo, mwandishi wa habari na Mkuu wa Wilaya wa zamani, ametumikia nafasi hiyo ya chama kwa miaka miwili na miezi saba, sehemu ya majukumu muhimu aliyotenda katika nafasi yake ni uchaguzi wa ndani ya chama.

Vilevile, katika mfumo wake wa utendaji, akitumia nguvu za chama kushika hatamu, amekuwa anafanya ziara za kitaifa na kuwawajibisha watendaji wa kiserikali, wakiwamo mawaziri.

Ni aina ya mtindo wa utekelezaji uliorithiwa hata na Katibu Mwenezi mpya, Paul Makonda, ambao walishafanya kazi pamoja mkoani Dar es Salaam, Chongolo akiwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni na Makonda Mkuu wa Mkoa.

Chongolo aliingia katika nafasi hiyo kurithi kiti cha Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Bashiru Ali, aliyedumu katika nafasi hiyo kwa miaka mitatu tangu Mei 2018. Akateuliwa kuwa mbunge.

Ndani ya ishara hiyo ya mageuzi ya kiutendaji ndani ya CCM inachukua nafasi huku kukiwapo angalizo la awali la Mwenyekiti Rais Samia Suluhu Hassan, akikiambia chama chake "tujipange kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani".

Chama hicho kimekuwa na desturi kinayoiita "kujivua gamba" unapokaribia uchaguzi mpya wa kitaifa, kikibadili baadhi ya viongozi wake, hasa kwa nafasi zenye ushawishi mkubwa kwa umma.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari juzi, Makonda alisema Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya CCM watakutana na vikao vya kawaida chini ya Mwenyekiti, Rais Samia.

Alisema kikao hicho kilitarajiwa kuanza na semina ya mafunzo kwa wajumbe wa Halmashauri Kuu na kufuatiwa na kikao cha Halmashauri Kuu Novemba 29 mwaka huu, yaani leo.

Makonda alisema kikao hicho ni cha kawaida. Kwa mujibu wa ratiba za chama, kunakuwa na vikao vikubwa viwili vya Halmashauri Kuu ambavyo vinakaa kwa mwaka; kimoja hufanyika mwanzoni mwa mwaka na kingine mwishoni mwa mwaka.


## TAARIFA KWA UMMA



117732002

Kampuni ya Hotels & Lodges (T) Limited inawataarifu wateja wake, Waendeshaji watalii na Umma kwa Ujumla kwamba Bw Aslam Anwar raia wa India (Pasipoti No.N2944608) mwenye picha hapo juu na aliyekuwa Meneja Mkuu kwenye mmoja ya vitengo vya Kampuni yetu ametoroka kazi kuanzia tarehe 01 Agosti 2023 na hahusiani tena na kampuni yetu. Tunapenda kutoa taarifa kwamba Kampuni yetu haitawajibika kwa matendo yake yoyote, miamala ya biashara au uidhinishaji kwa niaba ya kampuni yetu na watu wanaoshughulika naye watafanya hivyo kwa madhara yao wenyewe kwani kampuni yetu haitachukua jukumu lolote katika suala hili.

Utawala wa Hotels & Lodges (T) Limited, summit Centre, Arusha, Tanzania.


# UWT yatangaza itamkana Gekul, kashfa ikithibitika

**Na Beatrice Shayo**

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT) umeomba vyombo vya dola kuharakisha uchunguzi kuhusu tuhuma zinazomkabili aliyekuwa Naibu Waziri wa Sheria na Katiba, Pauline Gekul.

Vilevile, umoja huo umependekeza adhabu kali ichukuliwe dhidi ya kiongozi wao huyo endapo kashfa inayomkabili itathibitika.

Gekul ambaye ni Mbunge wa Babati Mjini (CCM), anatuhumiwa kutoa maelekezo kwa kundi la vijana kumdhalilisha kwa kumpiga, kumwingizia chupa sehemu za haja kubwa na kumtishia kumpiga risasi mfanyakazi wake, Hashim Ally.

Mwenyekiti wa UWT, Mary Chatanda, alisema jana kuwa wamepokea kwa masikitiko taarifa za tuhuma zinazomkabili Gekul kuhusu kumfanyia ukatili kijana huyo.

"UWT tunaomba vyombo vya dola kukamilisha uchunguzi kwa haraka ili kuleta imani kwa wananchi na kutoa pole kwa familia iliyoathirika," alisema.

Mary alisema endapo tuhuma hizi zikithibitika, hatua stahiki zichukuliwe ikiwamo adhabu kali ili iwe fundisho kwa viongozi wengine kufanya kazi zao kwa kuzingatia maadili ya uongozi.

"Sisi UWT tunazunguka nchi nzima kupinga na kukemea ukatili wa kijinsia na kuporomoka kwa maadili, hivyo tunapinga vikali kitendo hiki na endapo tuhuma hizi za mbunge zikithibitika, hatua stahiki zichukuliwe na adhabu kali zitolewe juu yake," alisema.

Mary alisema UWT haitavumilia kiongozi yeyote mwanamke atakayethibitika kufanya ukatili wa kijinsia na wanasisitiza umuhimu wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia viapo vyao, maadili ya uongozi na utawala bora.

Pia alisema UWT inampongeza Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti wa CCM kwa uamuzi wa kutengua uteuzi wa Gekul katika nafasi ya Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**Mary alisema endapo tuhuma hizi zikithibitika, hatua stahiki zichukuliwe ikiwamo adhabu kali ili iwe fundisho kwa viongozi wengine kufanya kazi zao kwa kuzingatia maadili ya uongozi.**

## Mfuko uwekezaji kuchochea ukuaji wa mashirika ya umma

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Msajili imeanza utekelezaji wa kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ambao utasaidia kimtaji mashirika ya umma na kuchochea ukusanyaji mapato ya serikali yasiyo ya kikodi.

Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam katika kikao kazi baina ya ofisi yake, waandishi wa habari na wahariri wa vyombo vya habari.

Mchechu alisema hatua hiyo inatokana na kuwasilishwa kwa Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Uwekezaji kwa Umma (PIA) katika kikao cha Bunge kilichomalizika mjini Dodoma hivi karibuni ambao pamoja na mambo mengine unaelezea kuanzishwa kwa mfuko huo.

"Muswada huo uliwasilishwa kwa mara ya kwanza Novemba, mwaka huu na unatarajiwa kusomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa na wabunge katika kikao cha Februari, mwakani. Tunachotakiwa kufanya ni kufumua menejimenti, kubadili uongozi, tutaangalia huko mbele," alisema.

Kwa mujibu wa Mchechu, Ofisi ya Msajili wa Hazina inawajibika kusimamia utendaji wa mashirika na taasisi zote za umma.

Hata hivyo, alisema wa sasa hakuna vyanzo vya fedha kwa ajili ya kuendesha mfuko huo na kwamba vitakuwa pamoja na sehemu ya maduhuli yatakayokusanywa na mamlaka, ambayo kiwango chake kitabainishwa kwenye kanuni.

Kwa sasa, taasisi na mashirika ya umma yaliyoko chini ya Hazina 248 ndani ya nchi, kampuni ambako serikali ina hisa chache 50, kati ya hizo za ndani ni 40 na nje 10.

Taasisi za umma kisekta, mamlaka za maji mabonde 43, elimu ya juu na mafunzo 42, usimamizi na usimamizi wa sekta 41, utalii 11, taaluma 11, mazao tisa, uendelezaji wa sekta saba, hospitali na vituo vya afya sita, mifuko ya hifadhi za jamii minne, udhibiti na ubora wa elimu minne, rufani za sheria minne na nyinginezo 51. Baadhi ya maeneo ambako serikali inamiliki hisa ni pamoja na Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE), Benki ya NMB, NBC na kampuni za TANRE na TDFL. Kwa nje ni Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (afDB), Shirika la Africa Re-Insurance na Benki ya Dunia (WB).

# Mtoto achomwa mikono madai kudokoa mboga

**Na Vitus Audax**

MTOTO Grace Mwita mwenye umri wa miaka mitano mkazi wa Mtaa wa Starehe, Tarime mkoani Mara, amechomwa mikono na baba yake mzazi akimtuhumu kuiba mboga hali iliyomsababishia maumivu na kuvimba mikono.

Akielezea tukio hilo jana, Mwenyekiti wa Mtaa wa Starehe, Mwita Ndagi, alisema alipokea taarifa za ukatili dhidi ya binti huyo kutoka kwa wananchi waliofika nyumbani kwake majira ya saa 12:00 asubuhi.

Mwita alisema baada ya kutoka kwa ajili ya kuwasikiliza, alimwona mtoto huyo aliyeambatana na wananchi hao, akiwa amechomwa mikono yote na imevimba, hivyo alipelekwa kituo cha polisi kwa ajili ya kupata fomu namba tatu (PF3) ya polisi kwa ajili ya matibabu pamoja na kutoa taarifa za mtuhumiwa huyo.

"Baada ya mtoto kuanza kupatiwa matibabu tulimpeleka pia mtuhumiwa huyo katika kituo cha polisi na kuchukuliwa maelezo kisha kuendelea kubaki polisi kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria," alisema Mwita.

Alisema kwa zaidi ya miaka mitano, tukio la namna hiyo ni la kwanza, hivyo kuiomba serikali kumchukulia hatua baba aliyetekeleza ukatili huo ili iwe fundisho kwa wengine wanaotaka kufanya hivyo.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo na mkazi wa Mtaa wa Starehe, Juma Danga, alisema awali alisikia mtoto huyo akilia wakati akifanyiwa kitendo hicho na baba yake na baada ya kilio kuzidi ilibidi aende kumzuia lakini aliendelea kumwadhibu.

"Nilikuta mtoto ameinua mikono juu akiwa anaendelea kumchapa mikono hiyo ambayo alikuwa tayari ameichoma lakini kwa wakati huo ilikuwa bado haijavimba, hivyo alinikatalia nikaamua kuondoka kwani ilikuwa usiku," alisema.

Akielezea hali ya binti huyo, bibi wa mtoto, Mkami Mwita, alisema mama wa mtoto huyo alimwacha akiwa na miaka mitatu na yeye ndiye anayewahudumia watoto pamoja na baba yao kwa kazi ya mgahawa.

"Nilivyotoka mgahawani nilikuta mtoto amelala akiomba msaada ndipo baba yake akaniambia leo tunakula ugali bila mboga, nikamuuliza inawezekanaje wakati nimeacha kila kitu, akasema mjukuu wako kaila ndipo nikagundua chazo za mtoto kulia," alisema bibi huyo.

Kuhusu hali ya mtoto, Mkami alisema baada ya kupelekwa hospitalini, alipatiwa huduma za awali na anaendelea kutumia dawa za maumivu ikiwa ni pamoja na sindano. Alisema hali yake si mbaya licha ya mikono kuwa bado imevimba.

Ikiwa ni siku ya tano sasa tangu uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia nchini, elimu na uelewa kwa jamii kuhusu matendo ya ukatili bado inaonekana kukosekana hali inayosabisha kuwapo kwa matukio endelevu ya ukatili dhidi ya watoto na wanawake hususani katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

**MATUKIO KUKITHIRI**

Matukio ya unyanyasaji dhidi ya watoto yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara katika maeneo mbalimbali nchini, mengi yakionyesha watoto kuchomwa moto au kujeruhiwa na wazazi au walezi wao.

Mkoani Kilimanjaro, mwanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Reli Juu, wilayani Mwanga, Shamshudin Msemo (13), alichomwa moto Agosti 31, mwaka huu, na mama yake mzazi kwa kile kilichodaiwa kuchukua fedha na kwenda kununua viazi vya chipsi kicha kuvipika baada ya kuhisi njaa.

Kutokana na kitendo hicho, mama alimfunga mikono na miguu mtoto huyo kisha kumtuma mtoto wa jirani kwenda kununua mafuta ya taa na hatimaye kummwagia na kumchoma kwa kiberiti. Mtoto huyo alilazwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Moshi, na kushindwa kufanya mtihani wa darasa la saba na hatimaye kupoteza maisha Oktoba 3, mwaka huu.

Aprili 7, mwaka huu, Grace Godwin (23) mkazi wa Mtaa wa SIDO, Manispaa ya Shinyanga, alitiwa mbaroni na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa tuhuma za kumchoma moto mikono mtoto wake wa miaka saba kwa madai kula kiporo cha ubwabwa bila ruhusa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UBORESHAJI WA MAJARIBIO (PILOT) WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA 'BIOMETRIC VOTER'S REGISTRATION (BVR) KUANZIA TAREHE 24/11/2023 HADI 30/11/2023 KATIKA KATA ZA IKOMA NA NG'AMBO**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa kata ya Ikoma iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, Mkoani Mara na Kata ya Ng'ambo iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Mkoa wa Tabora kuwa, Uboreshaji wa Majaribio (PILOT) wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utafanyika kwa siku saba kwa kila kituo.

1. **SIKU:** Wananchi watajiandikisha na kurobresha taarifa zao kuanzia siku ya Ijumaa tarehe 24 hadi Alhamisi 30 Novemba, 2023
2. **VITUO:** Uandikishaji wapiga kura utafanyika katika vituo vitakavyoainishwa na Tume.
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa kuanzia saa 2:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 12:00 kamili Jioni

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGAKURA UTAHUSISHA MAMBO YAFUATAYO; -**

1. Kuandikisha wapiga kura wapya waliotimiza umri wa Miaka 18 ambao ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria.
2. Kuandikisha wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 ifikapo uchaguzi Mkuu 2025.
3. Kuandikisha wale ambao wanazo sifa lakini hawakujiandikisha hapo awali.
4. Kuboresha taarifa za Wapiga kura waliohama Kata au Majimbo yao ya Uchaguzi au ambao taarifa zao zilikosewa hapo awali Mf. Majina
5. Kwa wale wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa binafsi na wanaohama vituo au vyote viwili kwa wakati mmoja wanaweza pia kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zao kwa kwa njia ya mfumo wa mtandao 'online'. Mfumo huu wa kuboresha taarifa za mpiga kura unapatikana katika mtandao wa Tume - www.nec.go.tz kwa kutumia kompyuta au simu janja kisha atabonyeza kiunganishi (link) iliyoandikwa "Boresha Taarifa za Mpiga Kura" au atatumia anuani ya ovrs.nec.go.tz itakayompeleka moja kwa moja kuanzisha mchakato huo. Katika mfumo huu, wapiga kura wanatakiwa kuingiza namba ya kitambulisho cha taifa (NIN), namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu anayotumia kwa sasa na jina la kata kisha watapata ujumbe wenye namba ya utambulisho (token namber) ambayo wataenda nayo kituoni ili kukamilisha taratibu za kupata kadi ya mpiga kura.
6. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura waliopoteza kadi zao au kuharibika.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kujiandikisha au kuboresha taarifa zao itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokuwa nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituoni atachukuliwa alama ya vidole vyote kumi vya mikono yote miwili na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Kwa Mpiga Kura aliyeboresha taarifa zake mtandaoni ni muhimu akahifadhi vyema namba ya kumbukumbu (token) ili iweze kumsaidia kupata kadi yake anapokwenda katika kituo cha kujiandikisha.

Tumia haki yako ya msingi kwa kwenda kujiandikisha.

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

217722802



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

**TANGAZO KWA UMMA**

**MIKOPO YA PEMBEJEO ZA UFUGAJI SAMAKI KWA VIZIMBA AWAMU YA PILI**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inakaribisha maombi ya mkopo wa masharti nafuu. Mkopo huo unalenga kutoa pembejeo za ufugaji samaki kwa vizimba kibiashara katika Ziwa Victoria. Mkopo utajumuisha vizimba vya mviringo vya plastiki na chuma vyenye kipenyo cha mita 6, 8 na 10; vifaranga vya samaki sato; na chakula cha samaki. Walengwa ni vyama vya ushirika/vikundi, makampuni na watu binafsi wanaokidhi vigezo.

Maombi yaambatanishwe na andiko la biashara pamoja na muhtasari wa kikao ulioridhia kukopa na ukomo wa madeni kwa vyama vya ushirika; barua ya dhamana kutoka halmashauri husika kwa vikundi; na dhamana ya mkopo kwa mtu binafsi na kampuni. Maelezo ya kina yanapatikana katika tovuti ya Wizara www.mifugouvuvi.go.tz, Ofisi za Uvuvi Halmashauri husika na Ofisi za Wizara zinazoshughulika na masuala ya Uvuvi.

Maombi yote yaidhinishwe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na kutumwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kabla ya tarehe 29 Januari, 2024 kupitia anuani ifuatayo;

**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**
**S.L.P 2847**
**40487-DODOMA**
**Simu: +255 26 23 22613**
**Baruapepe: ps@uvuvi.go.tz**

177330

# TAMWA yanyooshea kidole wahariri, mameneja ukatili vyombo vya habari

**Na Elizabeth Zaya**

UTAFITI uliofanywa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu umebaini kuwa wenye mamlaka kwenye vyombo vya habari ndio wanaoongoza kutenda unyanyasaji wa kijinsia kwa waandishi wa habari wanawake nchini.

Utafiti huo wa TAMWA uliolenga kuangalia hali ya unyanyasaji wa kijinsia katika vyombo vya habari, umetaja miongoni mwa wenye mamlaka wanaotenda ukatili huo wa kijinsia kwa wanawake ni wenye vyeo vya meneja, wahariri na wakurugenzi.

Mkurugenzi wa TAMWA, Rose Reuben, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa utafiti huo ulifanywa kwenye vyombo vya habari 22 katika mikoa mitano ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ambayo ni Dar es Salaam, Morogoro, Arusha, Mwanza, Dodoma na Zanzibar.

Alisema waandishi waliohusishwa katika utafiti huo ni 137 kutoka katika mikoa hiyo. Asilimia 77 ya waliohojiwa walieleza kuwa walipitia unyanyasaji wakiwa kwenye vyombo vya habari, huku asilimia 59 wakithibitisha kupitia vitendo hivyo kutoka ndani ya vyombo vya habari na asilimia 27 wakipitia unyanyasaji huo kutoka nje ya vyombo vya habari.

Rose alisema katika utafiti huo, pia walibaini kwamba ndani ya vyombo hivyo vya habari kuna unyanyasaji wa rushwa ya ngono na unyanyasaji wa maneno.

"Lengo la kufanya utafiti huu ni kutaka usalama wa waandishi wa habari katika eneo hili la unyanyasaji wa kijinsia uangaliwe na tunataka hata wao nao wafahamu jamii inawategemea katika kutoa taarifa za mrengo wa kijinsia.

"Unyanyasaji wa aina hii unachangia kwa kiwango kikubwa kupunguza idadi ya waandishi wa habari wanawake. Pia unasababisha jamii kukosa taarifa zenye mrengo wa kijinsia," alisema.

Akizunguma katika maadhimisho hayo, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Kundo Mathew, alisema asilimia 64 waandishi wa habari wanaume wana uhakika wa kupewa mikataba ya kazi na wanawake ni asilimia 36.

Pia alisema bado kuna idadi ya wanawake wanaoshika nafasi za juu za uongozi ikiwamo za mameneja kwenye vyombo vya habari kulinganisha na wanaume.

"Kwahiyo, serikali tuko tayari kupokea na kufanyia kazi maoni yoyote mtakayotuletea ikiwamo maboresho kwenye sera na sheria zinazosimamia vyombo vya habari," alisema Mathew. Pia alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uhuru wa kujieleza kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari nchini.

Mkurugenzi wa Klabu za Waandishi wa Habari nchini (UTPC), Kenneth Simbaya, alisema wameanzisha programu maalum ambayo miongoni mwa kazi zake ni kupita kwenye vyombo vya habari kuzungumza na kutoa elimu ya kupambana na vitendo hivyo vya unyanyasaji.

"Tunatambua madhara yanayowakuta waandishi wa habari wa kike ambayo pia yamekuwa yanawanyima fursa mbalimbali.

"Kwahiyo, sisi tumeanzisha utaratibu wa kuvifikia vyombo vya habari ambako matukio hayo yanaripotiwa na kuzungumza nao na tunajikita zaidi kuwaelimisha waandishi ili wawe wanaripoti," alisema Simbaya.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kulia), akikabidhi vifaa vya uvuvi kwa mmoja wa wanufaika wa mkopo wa boti, wakati wa kukabidhi boti kwa wavuvi wa Mkoa wa Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MOI yapoteza mil.300/- kila mwezi

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Tiba na Mifupa Muhimbili (MOI) imekuwa ikipoteza Sh. milioni 300 kwa mwezi kutokana na matibabu ya msamaha.

Kutokana na hali hiyo, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ameagiza kuchunguzwa kwa wagonjwa wanaopatiwa rufani kwenda kabla ya kupatiwa msamaha wa malipo kwa kuwa baadhi yao ni wadanganyifu.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizindua miradi ya kimkakati likiwamo jengo jipya la kliniki kwa wagonjwa maalum na wa kimataifa, jengo la kukaa wagonjwa, CT Scan na MRA na mwongozo wa dawa.

"Utakuta mgonjwa ameanzia hospitali binafsi huko wametumia fedha nyingi ndipo wanaamua kutoka na kwenda hospitali za mkoa ili wapatiwa rufani kwa ajili ya kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH)," alisema.

Alisema ni vizuri wagonjwa hao wakabainika walipoanzia matibabu yao na kama watokea hospitali binafsi watatakiwa kulipa fedha na si kutaka msamaha wakati huko walipotoka walikuwa wanalipa.

"Kila mwezi MOI inasemehe Sh. milioni 300 halafu watu wanasimama ukiwa maskini hutibiwi. Naomba Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Abel Makubi, nijue hizo Sh. milioni 300 ni vipimo, dawa, upasuaji ama kulazwa.

"Natoa maelekezo kwa vituo vyote vya afya nchini. Tumepata kesi ya Kabuku juzi tumeambiwa mama ameshindwa kujifungua kwa sababu hana fedha ya kufanyiwa upasuaji Sh. 50,000 si kweli aliambiwa atafanyiwa upasuaji ila itabidi uchangie Sh. 150,000. anatafutwa mtaalamu wa huduma za usingizi na ganzi, je, daktari atamfanyia upasuaji bila ganzi tulionekana wote hatuna huruma sio kweli katika hilo," alisema.

Waziri alisema kabla ya Desemba atatoa takwimu ya misamaha iliyotolewa na serikali katika hospitali zake wataanza na za rufani, kanda na taifa.

Pia alisema kwa kuwa wamejitanua kutoa huduma za kimataifa ni vizuri wagonjwa wanaotoka nje ya nchi wapokewe vizuri kuanzia wanapofika kwenye viwanja vya ndege.

Alisema huduma hiyo waendeshe kwa ubia kwa kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha kunakuwa na mapinduzi katika huduma za afya ili ziwe za kiwango bora.

"Lazima tuwe na huduma bora kwa wateja tangu mgonjwa anapofika uwanja wa ndege hadi anafika hapa MOI, tushirikiana na sekta binafsi wawe wanawapokea hao wagonjwa si daktari ndio aanze kuhangaika naye au kuanza kumtafutia hoteli. Hiyo kazi ifanywe na sekta binafsi, lengo wagonjwa wafurahie huduma zetu," alisema.

Pia alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukizwa jambo ambalo linatakiwa kupewa uzito wake ili afya za wananchi ziwe salama.

Mwenyekiti wa Bodi ya MOI, Prof. Charles Mkony, alisema kumekuwa na changamoto ya wagonjwa wengi kuomba msamaha wa malipo na kujikuta kwa mwezi inafika hadi Sh. milioni 300.

Mkony alimwomba Waziri Ummy kuona namna ya kuwasaidia katika malipo hayo ili kupunguzia mzigo wa taasisi. Alisema tatizo lingine bodi kutokuwa na wajumbe kwa miaka miwili, hivyo ameomba jambo hilo kufanyiwa kazi.

Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abbas Tarimba, alisema anafurahishwa na huduma zinazotolewa na hospitali hiyo na kutaka wale wote ambao wametoa mchango wao kwa kufanikisha MOI kufika ilipo wawekwe kwenye maandishi ili wazidi kufahamika.

Naye mfanyabiashara na mdau wa masuala ya afya, Azim Dewji, alisema ataendelea kuwa mdau muhimu katika hospitali hiyo kwa uchangiaji wa damu salama huku akimwambia Tarimba kuweka mechi ya kirafiki baina ya Yanga na Simba ili fedha zitakapatikana zisaidie mchango unaotakiwa wa Sh. milioni 350 kwa uboreshaji wa huduma za wagonjwa wa nje MOI.

# Mvua yasababisha vifo watu wanane

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MVUA kubwa inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini, imesababisha vifo vya watu wanane mkoani Tanga.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi Almuchius Mchunguzi alitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari jana ofisi kwake, akifafanua kuwa watu hao wamekufa maji katika matukio tofauti kwenye wilaya za Tanga, Muheza, Handeni na Kilindi.

Aliwataja watu hao kuwa ni Fabius Masalu (23), mkazi wa Kijiji cha Ngomeni na Mbwana Hamisi Makame (48) ambaye alikuwa mgonjwa wa akili, alikufa maji katika Kijiji cha Kicheba, vyote vya wilayani Muheza.

Wengine waliofariki dunia ni mwanafunzi wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Maweni jijini Tanga, Abubakar Said (7) na Simon Arod (3) pamoja na mtoto mwingine mwenye umri wa miaka minane, Nganahe Masefu, mkazi wa Kijiji cha Mbwagwi wilayani Handeni.

Kamanda Mchunguzi aliwataka wananchi wanaoishi katika maeneo ya mabondeni kuchukua tahadhari na mvua inayoendelea kunyesha ili kuepuka madhara ikiwamo vifo.

"Mvua inayonyesha imesababisha vifo vya watu wanane katika mkoa wetu, watu wachukue tahadhari za kiusalama kipindi hiki cha mvua ikiwezekana wahame maeneo ya mabondeni," aliagiza kamanda huyo.

Pia alisema jeshi hilo limekamata watuhumiwa 107 katika msako waliofanya kwa kipindi cha mwezi mmoja. Wamekamatwa kutokana na tuhuma za makosa mbalimbali ikiwamo kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya; bangi kilo 43, mirungi kilo 123.5 na heroin gramu 242.

Kamanda huyo alisema kuwa Novemba 18 mwaka huu walimkamata Hamisi Kombo, mkazi wa Kwediboma wilayani Kilindi na wenzake wanne wakidaiwa kujifanya waganga wa kienyeji, wakipiga ramli chonganishi katika Mtaa wa Pongwe jijini Tanga.

Kamanda Mchunguzi alisema watuhumiwa 41, kesi zao zimepelekwa mahakamani na nyingine 11 jeshi hilo linaendelea na uchunguzi kabla ya watuhumiwa kufikishwa mahakamani.

Alisema jeshi hilo linawashukuru raia wema kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika nyanja mbalimbali ikiwamo kutoa taarifa ambazo zimefanikisha kukamatwa baadhi ya wahalifu pamoja na mali zilizoibwa.

HABARI KITAIFA

# China kuboresha miundombinu Dar

**Na Gwamaka Alipipi**

MIUNDOMBINU ya Mkoa wa Dar es Salaam inakwenda kuwa ya kisasa na bora. Uongozi wa mkoa umeingia hatua za awali za ushirikiano wa uendelezaji na Jiji la Shaanxi la China.

Makubaliano hayo pia yanalenga ushirikiano wa kitaifa ikiwamo uwekezaji katika viwanda, biashara, madini, kilimo, elimu, afya, utalii.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanyika makubaliano hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema makubaliano hayo ya awali yanakwenda kulinufaisha taifa kiuchumi na Mkoa wa Dar es Salaam hususani katika uendelezaji miundombinu.

Alisema baada ya makubaliano hayo ya awali, baadaye watatia saini hati ya makubaliano (MoU) kati ya Tanzania na China ambayo itawezesha kuanza utekelezaji wa makubaliano hayo.

"Sote tunafahamu Jiji la Shaanxi lilivyoendelea kimiundombinu na ndilo jiji analotoka Rais wa China, hivyo kuingiwa kwa makubalinao haya kutawezesha Mkoa wa Dar es Salaam kuwa na miundombinu ya kisasa kwa sababu wataalamu kutoka China watakuja kufanya uwekezaji katika miundombinu.

"Hapa kumefanyika makubaliano ya awali, baadaye mikataba itapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye atapitia kisha kutafanyika MoU," alisema.

Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN), Mkoa wa Dar es Salaam ifikapo mwaka 2030, utakuwa ni moja ya majiji saba duniani ambayo yana wakazi wengi na utakuwa ni mkoa wenye mwingiliano wa watu kutoka mataifa mbalimbali.

Chalamila alisema kwa ushirikiano uliongiwa na Jiji la Shaanxi, kutawezesha kuwa na miundombinu ya kisasa na ya uhakika.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alisema ushirikiano wa Tanzania na China ni wa historia na ulianza tangu utawala wa marais Hayati Julius Nyerere na Mao Tsetong.

Alisema ushirikiano China na Tanzania umekuwa na mafanikio mengi hususani katika nyanja za kiuchumi na kibiashara. Wafanyabiashara wengi kutoka Tanzania wamekuwa wakienda China kuchukua bidhaa.

Mingjian alisema Jiji la Shaanxi limeendelea na kupiga hatua kubwa katika miundombinu, hivyo ushirikiano huo unakwenda kuliwezesha Jiji la Dar es Salaam kupanuka na kuwa la kisasa zaidi.

Alisema ushirikano katika sekta za madini, elimu, biashara, afya na mengineyo unakwenda kulinufaisha Jiji la Dar es Salaam kwa sababu wataalamu kutoka China watakuja Tanzania na kuwekeza katika sekta hizo.

# Mkenda: Ubora wa vyuo vikuu Afrika uimarishwe

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amewataka Wathibiti Ubora wa Elimu ya Juu Barani Afrika (AfriQAN) kuimarisha ubora wa vyuo vikuu na kuvisimamia vibadilishane wahadhiri na wanafunzi na kufanya utafiti wa matatizo yanayokabili bara hilo.

Aliagiza hayo jana jijini Dar es Salaam alipofungua kongamano la siku tatu la AfriQAN na kusisitizia wasikubali ubora wa vyuo vikuu kushuka kwa namna yoyote.

Kongamano hili ambalo ni kwa mara ya kwanza kufanyika Tanzania, limeandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa kushirikiana na AfriQAN kwa lengo la kujadili mchango wa uthibiti ubora katika kuongeza umahiri wa elimu ya juu barani Afrika.

Prof. Mkenda alisema, "shinikizo la kushusha ubora siku zote lipo, lakini lazima tuhakikishe kwamba hatujatofautiana na nchi nyingine duniani. Tukumbuke uendeshaji wa vyuo vikuu ni biashara ya ushindani, vyuo vikuu katika ufundishaji wake ni kuhakikisha wanafunzi wanafanya vizuri."

Alikumbusha suala la kuajiri wahadhiri na vipo vigezo vyake na kusisitiza kuwa katika ushindani wa kibiashara kusiwe na presha ya kushusha vigezo ili kusema chuo kina maprofesa.

Kuhusu utafiti, waziri huyo alisema mtu hawezi kuwa mhadhiri chuo kikuu kwa kutoa mhadhara tu, ni lazima afanye utafiti.

"Ni lazima tushirikiane pia kwenye masuala ya utafiti huwa yanasaidia sana. Mfano sisi tumekuwa na tatizo kubwa la malaria, lakini Ulaya ni kama hawana tatizo hili. Tutakapofanya utafiti wa changamoto zetu itasaidia kuondokana nazo kwa kuwa wenzetu wanaweza wasiwe na msukumo mkubwa wa kuzifanya.

"Kuna suala tunasema tumeongeza wanafunzi vyuo vikuu, lakini suala la ajira limekuwa na changamoto. Kuna suala la vyuo vikuu ubora wake kupimwa kwa kiasi gani utamwandaa mwanafunzi aweze kujiajiri au kuajirika kirahisi," alisema.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema mkutano huo ni wa mtandao wa wathibiti ubora barani Afrika ambao ulianzishwa Novemba 27, 2009.

Prof. Kihampa alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufungua milango ya nchi na kuwezesha kufanyika kwa mikutano mingi.

"Mtandao huu wa wathibiti ubora barani Afrika ni muhimu kwa kuwa, wanashirikiana na wathibiti ubora mbalimbali barani humu katika kuthibiti ubora wa elimu kuanzia elimu ya msingi mpaka elimu ya vyuo vikuu," alisema na kubainisha mkutano huo una taasisi kutoka nchi 22 barani Afrika na tatu kutoka nje ya bara hilo.

# Balozi awapa angalizo waandishi wa habari

**Na Grace Gurisha**

BALOZI wa Uswisi nchini, Didier Chassot amewataka waandishi wa habari wa Tanzania kuripoti habari kwa njia inayolenga msingi wa kijinsia ili kusaidia kuondoa changamoto mbalimbali katika jamii.

Alitoa rai hiyo jana katika sherehe ya kuhitimu washiriki 10 (waandishi wa habari) katika programu ya mpango wa uvumbuzi wa kidijitali 'Digital Media Innovation Program' (DMIP) iliyofanywa na Kampuni ya Jamii Media jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa yeye hayupo kwenye nafasi ya uandishi wa habari, lakini anashauri waandishi wa habari kuandika habari zenye mrengo wa kuigusa jamii na pia kutokuogopa kusimamia misingi ya kazi zao.

"Tumieni mlichokipata hapa katika mafunzo mliyoyapata kuisaidia jamii. Ninajua kazi ya uandishi wa habari ina misukosuko sana duniani kote, lakini mnatakiwa kusimama imara kwa sababu kazi hii ni ngumu, ni lazima mpambane na changamoto mnazokutana nazo kwa lengo la kuisaidia jamii," alishauri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jamii Media, Mike Mushi, alisema kuwa Mei Mosi mwaka jana, ushirikiano wenye tija wa miezi 18 ulianza kati ya Ubalozi wa Uswisi na Jamii Media hiyo ukiwa na lengo la kuimarisha ujuzi wa majukwaa ya vyombo vya habari mtandaoni.

"Nia ni kujenga vyombo vya habari vya mtandaoni vyenye sifa nzuri vinavyoripoti kuhusu masuala ya kweli, yasiyo na upendeleo na yanayohusiana na maslahi ya umma.

"Jamii Media imechukua jukumu la kutoa mafunzo, kutoa msaada wa uzalishaji pamoja na msaada wa kiufundi," alisema Mushi.

Alibainisha kuwa katika mradi huo, walipokea maombi 430, asilimia 33.3 ni kutoka kwa wanawake na asilimia 66.7 kutoka kwa wanaume. Miongoni mwa waombaji, asilimia 57.8 hawakuwa wamiliki wa vyombo vyao vya habari za mtandaoni na asilimia 42.2 waliripoti kuwa wamiliki.

"Katika siku ya leo ya kusherehekea kumaliza mradi waandishi wa habari 10 wa vyombo vya habari mtandaoni wamepokea vifaa vya uzalishaji kitaalamu zikiwamo kompyuta mpakato, kamera, stendi ya kamera na vingine ambavyo vitawasaidia katika kazi zao," alisema.

Mmoja wa wanufaika hao ni Mukrim Khamis kutoka Zanzibar, alisema mafunzo yamemsaidia kufanya kazi zake kwa usalama zaidi na kusaidia jamii kutokana na changamoto zinazoikabili.

Jane Edward kutoka Arusha aliishukuru kampuni ya Jamii Media kwa kuwapatia mafunzo hayo ambayo yameleta mabadiliko katika jamii kuamini taarifa za mtandaoni kuwa ni za kweli. Wengi huwa wanajua taarifa za huko ni za uongo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 27-11-2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO** tarehe **29-11-2023** kampuni za **TRANSCARGO LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **TUNDUMA.** Gari hilo lenye namba za usajili:

**T 937 DUM / T 201 EAZ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **UREFU - MITA 20**
   **UPANA - MITA 4.3**
   **KIMO - MITA 4.8**

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi **TUNDUMA** kupitia **MOROGORO.**
   Gari itasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:30 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza

177318



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 27-11-2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO** tarehe **29-11-2023** kampuni za **TRANSCARGO LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **TUNDUMA.** Gari hilo lenye namba za usajili:

**T 724 DZX / T 583 DFL**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **UREFU - MITA 22**
   **UPANA - MITA 4.3**
   **KIMO - MITA 4.8**

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi **TUNDUMA** kupitia **MOROGORO.**
   Gari itasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:30 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza

177318

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Siku 16 za kupinga ukatili, jamii ioneshe kwa vitendo

**TAASISI** mbalimbali zisizo za kiserikali na kiserikali zikiwa kwenye maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili, vitendo hivyo vinaendelea kushamiri katika baadhi ya maeneo.

Licha ya elimu inayotolewa na uhamasishaji wa kupinga vitendo hivyo, bado kuna watu wanafanya unyama kwa kuwafanyia ukatili binadamu wenzao.

Katika siku za karibuni kumeibuka vitendo hivyo, na baadhi wanaovifanya kugundulika wengine kuwa na tatizo la afya ya akili.

Katika kutekeleza siku 16 za kupinga ukatili kuna kila sababu kwa jamii kuhakikisha inafuatilia mienendo ya ndugu zao wanaoishi nao ili kugundua kama kuna dalili zozote zinazoashiria mtu kuwa na tatizo hilo aweze kuchunguzwa na kupatiwa tiba.

Ni hivi juzi tu kuliporipotiwa taarifa za mtu kukata vichwa vya binadamu wenzake na kisha kuondoka navyo na baadaye kugundulika kuwa mtu huyo alikuwa na tatizo la afya ya akili.

Kuna wengi wanafanya vitendo hivyo wakiwa na akili timamu, lakini kwa sababu wanapenda kuonea binadamu wenzao wanawatesa kwa kuwafanyia ukatili.

Katika tukio lingine mtoto mmoja wenye umri wa miaka mitano mkoani Mara amechomwa mikono na baba yake mzazi akimtuhumu kuiba mboga.

Mwenyekiti wa Mtaa alipokea taarifa za ukatili dhidi ya binti huyo kutoka kwa wananchi waliofika nyumbani kwake.

Wananchi hao walikuwa na mtoto huyo akiwa amechomwa mikono yote ikiwa imevimba.

Matukio hayo yanatokea mara kwa mara na wahusika wakuu huwa ni ndugu wa karibu au wazazi, jambo linalofikirisha kwanini mzazi aamue kuchukua uamuzi huo.

Sababu kubwa inayotolewa ni hali ngumu ya kiuchumi ambayo hata hivyo, haiingii akilini kwa kuwa mtoto ulimzaa kwa uchungu ukampa mateso kama hayo.

Pamoja na kuwekwa madawati ya jinsia, bado kuna maeneo mengine vitendo hivyo haviripotiwi na matokeo yake kuendelea kufanyika katika jamii.

Jamii inapaswa kuchukua hatua kwa kutoa taarifa kila mara matukio hayo yanapojitokeza ili wahusika wachukuliwe hatua na iwe fundisho kwa watu wengine. Baadhi ya watu huamua kuingilia kati wanaposikia matukio hayo ya ukatili yakijitokeza ili kudhibiti hali ya ukatili isiendelee.

Hatua hii husaidia kumuokoa anayefanyiwa ukatili ili asipate madhara makubwa. Na pia anayefanya kitendo hicho huogopa kuripotiwa polisi.

Baadhi ya walezi huamua kuwachukua watoto wa ndugu zao wakidai kwenda kuwasaidia kuwasomesha, lakini wanapofika majumbani kwao huwanyanyasa kwa kuwafanyia ukatili wa kinyama.

Matukio ya ukatili yanaripotiwa zaidi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na hivyo elimu endelevu inatakiwa kutolewa ili kudhibiti hali hiyo.

Leo ni siku ya tano sasa tangu uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia nchini, licha ya elimu na uelewa kwa jamii kuhusu vitendo hivyo bado inaonekana matukio hayo kuwa endelevu dhidi ya watoto na wanawake husuani katika mikoa hiyo.

Kisingizio cha hali ngumu ya uchumi hata mtoto anapodokoa mboga badala ya kumkanya kwa maneno na kuchukua uamuzi wa kumuunguza kwa moto mikono au kumchanja kwa wembe, ukatili huo haukubaliki na unapaswa kukemewa kwa nguvu zote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Golden Kisapile, TUDARCO.

# Hii ni dawa ya utapeli wa sms

**UTAPELI** wa ujumbe mfupi au SMS unaotumwa na simu unaendelea kuumiza wengi iwe mjini au vijijini na baadhi wakihoji, au kuna jambo?

Kwanini wahusika wasidhibitiwe kama namba zote zimesajiliwa na ambazo hazina utambulisho zimefungiwa? Hata mimi sina jibu.

SMS inayosema nitumie pesa kwa namba hii, imeumiza wengi na kusababisha hasara kubwa kifedha na hata kihisia na pengine hata vifo.

Hata mimi napata wasiwasi kuhusu ongezeko la utapeli wa mtandaoni, watu wakilizwa baada ya kupokea SMS au kupigiwa simu na matapeli wanaoleta hoja nyingi mbalimbali.

Mfano kuna wanaoeleza wazazi na walezi kuwa watoto wao walioko bweni wanaumwa na wanahitaji fedha za matibabu. Wengine wanadanganywa wametumiwa kiasi kikubwa cha fedha na kutakiwa kukirejesha. Pia wameshinda bahati nasibu hivyo walipie kidogo wachukue mamilioni yao.

Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa utapeli huu umeshika kasi hata baada ya kusajili namba kwa bayometria au kutumia alama za vidole.

Ili kudhibiti au kukomesha aina hii ya utapeli, pengine hatua hizi zingesaidia mosi, serikali kushirikiana na watoa huduma za simu na vyombo vya sheria kufuatilia na kukamata wahusika wa utapeli huu.

Aidha, kuanzishwa kwa sheria na adhabu kali kwa wale wanaopatikana na hatia, kadhalika elimu na uelewa wa umma ni muhimu ili wananchi waelewe mbinu za utapeli wa mtandaoni na jinsi ya kujikinga.

Kampeni za elimu zinaweza kufanywa kupitia vyombo vya habari, shuleni na taasisi nyingine za umma na zisizo za kiserikali ili kuwafahamisha watu hatari na mbinu za utapeli huo.

Aidha, watoa huduma za simu za mkononi wanaweza kuchukua hatua za kuboresha usalama wa mitandao yao na kutoa mafunzo kwa wateja juu ya kuepuka utapeli wa mtandaoni.

Kushirikiana na Wakala wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na kuweka njia za kudhibitisha utambulisho wa wateja wanaoeneza ujumbe wa matapeli ni hatua muhimu kupambana na tatizo hilo.

Ushirikiano kimataifa nao ni mbinu kwa kuwa utapeli wa ujumbe wa simu ni tatizo la kimataifa, ushirikiano kudhibiti haukwepeki.

Serikali inapaswa kushirikiana na nchi nyingine na mashirika ya kimataifa kubadilishana taarifa za uhalifu, kupeana uzoefu na kufanya kazi pamoja katika kudhibiti utapeli wa SMS.

Teknolojia ya kuzuia, kwa kushirikiana na mitandao ya simu ni vyema kubuni au kuweka mifumo ya kiteknolojia ya kuzuia ujumbe wa utapeli usifike pale unapotumwa na kuundoa kwenye uwanja.

Hii inaweza kujumuisha matumizi ya teknolojia ya kugundua na kuzuia ujumbe wa utapeli au kuanzisha mifumo ya kufuatilia na kuchunguza utapeli huo na kuuondoa kwenye mawasiliano.

Elimu ya kuepuka kutoa taarifa za siri iendelee ili wenye simu wasiwape watu ambao hawawajui taarifa za binafsi na za siri kama vile namba za akaunti, neno la siri au namba ya kitambulisho

kujihadhari na yeyote anayeleta ombi ya kutaka taarifa binafsi na watu wasiamini mazungumzo ya simu.

Ni vyema kuelimisha wengine; kushirikiana maarifa lakini kueleza familia na marafiki kuhusu hatari za utapeli wa SMS na jinsi ya kujikinga ili waweze kuwa macho.

Wakati mwingine ni kutumia mitandao ya kijamii kutoa taarifa na ushauri kuhusu utapeli wa SMS mitandaoni ili kuwafikia watu wengi zaidi.

Lakini pia ni vyema watu kutumia neno siri gumu, weka maneno, namba , alama kwa mfano ' '@j1o234?*' kuzuia watu wasiweze kufikia simu yako na kukuibia.

Lakini ukiwa na simu janja hakikisha unatumia programu za usalama, za kulinda simu yako kutokana na virusi kusaidia kuzuia utapeli wa SMS ikibidi tumia 'true caller app'.

Aidha, ripoti utapeli kwa kuwasiliana na mtoa huduma ili waweze kuchukua hatua za haraka lakini pia fikisha ujumbe ripoti kwa maofisa wa Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano (TCRA) ili waweze kuchunguza na kuchukua hatua.

Elimisha wengine, shirikiana maarifa yako, eleza familia na marafiki hatari za utapeli wa SMS na jinsi ya kujikinga ili waweze kuwa macho.

## HABARI KITAIFA

# Umeme warejeshwa Muheza, transfoma mpya yafungwa

**Na Steven William,** MUHEZA

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) wilayani Muheza mkoani Tanga limerejesha huduma ya umeme kwa wateja wake kwa kufunga transfoma nyingine baada ya ile ya awali 'kupiga shoti' kuungua na kusababisha wananchi kukosa huduma kwa siku tatu.

Transfoma hiyo ilipiga shoti na kuungua usiku mwishoni mwa wiki iliyopita kutokana na mvua katika Mtaa wa Masaki Misufini wilayani Muheza.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Muheza, Chuwa African alisema wameweka transfoma mpya katika eneo hilo na kutoa ile ya zamani iliyoungua.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji wa Muheza, Seif Twenye alimpongeza meneja huyo kwa kurejesha huduma haraka kwa kuwa wamezoea kunapotokea tatizo kama hilo wanakaa muda mrefu, hata mwezi mzima pasi na huduma ya umeme.

Meneja huyo wa TANESCO alisema transfoma hiyo ilipiga shoti na kuungua usiku na hivyo wateja kukosa umeme. Jitihada zilifanyika na hatimaye kupata transfoma kwa haraka na kurejesha huduma kwa wananchi.

Alibainisha kuwa karibu vijiji vyote katika Wilaya ya Muheza vimeshafikiwa na huduma ya nishati ya umeme.



Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Benki ya Azania, Charles Mugila, akizungumza baada ya benki hiyo kutiliana saini makubaliano ya ushirikiano wa kiutendaji na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watalii viziwi watembelea Hifadhi ya Taifa Mikumi

**Na Nebart Msokwa,** MOROGORO

WATALII 165 ambao ni viziwi kutoka mataifa mbalimbali duniani, wametembelea Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA) mkoani Morogoro kwa lengo la kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vinavyopatikana ndani ya hifadhi hiyo.

Watalii hao walifanya ziara hiyo juzi wakitokea mkoani Dar es Salaam ambako walikuwa na mkutano ulioambatana na michezo mbalimbali yakiwamo mashindano ya ulimbwende na utanashati.

Kaimu Meneja wa Uhusiano wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Robert Masunya alisema waliamua kuwapeleka watalii katika hifadhi hiyo kama sehemu ya kuitangaza.

Alisema watalii hao wanatoka mataifa zaidi ya 40 yakiwamo ya Bara Asia, Ulaya na Amerika na hivyo wakirudi kwao ni rahisi kusimulia aina ya vivutio vya Tanzania na kuhamasisha wenzao kuja kuvitembelea.

"Utalii huu ni wa pekee kwa sababu unahusisha kundi kubwa la watu wenye usikivu hafifu (viziwi) na wamechanganyika Watanzania na wageni kutoka mataifa mengine," alisema Masunya.

Mkuu wa MINAPA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Ignas Gara, alisema watawatembeza watalii hao katika maeneo mbalimbali ili wajionee vivutio vilivyomo.

Alisema watawaonyesha makundi mbalimbali ya wanyama wakiwamo simba, swala, twiga, tembo, nyati na makundi ya ndege waliomo ndani ya hifadhi hiyo.

Alisema Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limewaandaa waongoza watalii ambao wana uwezo wa kuwasiliana na makundi mbalimbali ya watalii wakiwamo viziwi.

Baadhi ya watalii hao walisema Tanzania ni miongoni mwa maeneo ambayo yanavutia duniani ambayo yanavutia kuishi kutokana na amani iliyopo.

Kiongozi wa viziwi kutoka Hispania, Marina Rogares, alisema yeye na wenzake alioongazana nao kutoka nchini kwao, ni mara yao ya kwanza kufika Tanzania na barani Afrika kwa ujumla.

Alisema tangu walipofika nchini, walibaini Watanzania ni wakarimu na wasiokuwa na ubaguzi kwa makundi maalum, ni hali iliyowafanya wafurahie zaidi.

# 'Tuhifadhi maeneo ya kihistoria'

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI wa Malikale - Makumbusho amewataka Watanzania kujenga utamaduni wa kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti na kutunza sehemu zenye maeneo ya kihistoria.

Jijini Dar es Salaam juzi, Revocatus Bugumba alitoa rai hiyo alipokutana na wawakilishi wa Jiji la Hamburg, Ujerumani waliozuru nchini kwa ajili ya kuendesha semina ya upandaji miti, maua, utunzaji bustani na mazingira.

Alisema Dar es Salaam na Hambarg ni majiji yenye urafiki na kwa muda mrefu yamekuwa yanasaidiana kwenye mambo mengi yahusuyo mazingira.

Alisema wageni hao watakuwapo nchini hadi Ijumaa ijayo kwa lengo la kubadilishana uzoefu namna ya kutunza bustani na mazingira, akisitiza wageni wao hao wana uwezo mkubwa kwenye eneo hilo.

"Utunzaji mazingira na bustani una faida nyingi sana; unaongeza ajira, wakati mwingine hata kupumzika tu wataalamu. Wanasema ukipumzika kwenye kivuli safi ni tiba kwa afya.

"Kwa mfano hapa Dar es Salaam, kuna upungufu wa maeneo ya kupumzika, lakini tukijenga utamaduni wa kuwa na sehemu nzuri zilizotengenezwa kwa mpangilio na kuweka bustani, watu watakuja kupumzika na kupata hewa safi baada ya vurugu mbalimbali za kazini," alisema.


Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Jiji la Hamburg, Dk. Ana Sebode, alisema ushirikiano kati ya Tanzania na Ujerumani kwenye eneo la mazingira umekuwa na mafanikio makubwa na umeleta tija.

Aliahidi kwa muda watakaokuwa nchini kuendesha mafunzo hayo, wanatarajia kubadilishana uzoefu na Watanzania ili wenyeji wao hao wawe vizuri kwenye eneo hilo kwa kuwa wameambatana na wataalamu kutoka nchini kwao.

Aliwaomba wadau na wananchi kujitokeza kwa wingi kuanzia kesho mpaka Ijumaa ya juma hilo kuhudhuria mafunzo hayo yanayofanyika katika Ukumbi wa Makumbusho ulioko Posta jijin Dar es Salaam.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Watu 23 wauawa na tembo

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

WATU 23 katika Kijiji cha Mangae wilayani Mvomero, mkoani Morogoro, wameuawa na tembo katika matukio tofauti yaliyotokea katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013 hadi 2023 katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi (MINAPA).

Mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima kwenye mkutano na wananchi, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mangae, Belege Alex, alisema jana kuwa tembo hao waliosababisha vifo hivyo, pia wametajwa kufanya uharibifu ikiwamo kubomoa nyumba na kuharibu mazao mbalimbali ya wakulima katika kijiji hicho na vijiji vya jirani.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, kero kubwa inayotusumbua, mpaka sasa watu 23 wameuawa na tembo wanaovuka kutoka Hifadhi ya Taifa Mikumi kuja hapa kijijini kwetu. Pia wameharibu mazao katika mashamba yetu. Tunaomba jambo hili lipatie ufumbuzi," alisema.

Alisema ni kero ya muda mrefu. Wamejaribu kuifikisha kwa uongozi wa MINAPA, lakini haijapatiwa ufumbuzi.

Kamishna wa Uhifadhi Kanda ya Mashariki wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Masana Mwishawa, alithibitisha kuwapo changamoto ya tembo kutoka hifadhini na kwenda kufanya uharibifu katika makazi na mashamba ya vijiji jirani.

Kamishna Mwishawa alisema tayari suala hilo wameliwekea mkakati ikiwamo kuweka askari wa TANAPA kwenye mipaka na maeneo yaliyo karibu na vijiji hivyo ili kuwarudisha hifadhini wanyama wote wanaotaka kutoka nje ya hifadhi kwenda kwenye makazi ya watu.

"Mikakati yetu mingine ni pamoja na kufundisha vijana wanaoishi kwenye vijijini jirani na hifadhi yetu kwa kuwapa mbinu za kuwadhibiti wanyama wakali kwa ushirikiano na askari wetu wa hifadhi na mpaka sasa vijana 28 wameshapatiwa mafunzo," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, akizungumza na wananchi wa kijiji hicho, alisema hakubaliani na hali hiyo, akiwaagiza TANAPA kudhibiti wanyama hao wasitoke ndani ya hifadhi na kuwekeza kwenye ujirani mwema na wananchi.

"Panapotokea tatizo hilo la wanyama, ninyi TANAPA mnapaswa kukimbia haraka kwenda kwenye vijiji hivyo kuwasikiliza, huo ndio ujirani mwema kwani wananchi wanapaswa kusikilizwa na kutatuliwa matatizo yao kwa haraka," aliagiza.




Meneja Msimamizi wa Huduma za Uwezeshaji na Upatikanaji wa Vodacom Tanzania Plc, Edward Byampanju (mwenye jezi nyeupe), akifafanua jambo kwa mawakala wa kampuni hiyo, walipotembelea makao makuu ya kampuni hiyo nchini Afrika ya Kusini hivi karibuni. Ziara hiyo ni matokeo ya jitihada za kampuni hiyo za kuwazawadia mawakala wake kutokana na utendaji bora wa kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TMDA yatoa ufafanuzi dawa ya Carbotoux

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kupitia Mkurugenzi Mkuu wake, Adam Fimbo, imetolea ufafanuzi kuhusu taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kuwapo dawa aina ya Carbotoux (Carbocisteine 100mg + Promethazine 2.5mg).

Kwa mujibu wa taarifa ya mkurugenzi huyo iliyotolewa juzi, dawa hiyo inatengenezwa na Kampuni ya Labotatories P.P.M, Cambodia katika soko la Tanzania.

"Hivi karibuni kumekuwa na taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zikihusisha kuwapo dawa duni yenye jina Carbotoux (Carbocisteine 100mg + Promethazine 2.5mg) katika soko la Tanzania.

"Taarifa hiyo inaainisha kuwa dawa tajwa husababisha madhara makubwa kwa watumiaji na hivyo si salama kwa matumizi ya binadamu," mkurugenzi huyo alieleza katika taarifa yake hiyo.

Hata hivyo, alisema TMDA inauhakikishia umma kuwa dawa yenye jina Carbotoux haijawahi kusajiliwa kwa matumizi nchini.

Vilevile, alisema kampuni ya Labotatories P.P.M, Cambodia inayotengeneza dawa hiyo, haijasajili dawa yoyote nchini.

Alisema TMDA imesajili dawa zenye kiambata cha Carbocisteine + Promethazine zinazotengenezwa na kampuni zingine. Dawa hizo ni bora, salama na fanisi kwa matumizi yaliyokusudiwa.

"Mamlaka imeimarisha udhibiti wa mifumo ya ufuatiliaji wa dawa katika soko (post marketing surveillance) ili kubaini kuwapo dawa duni zikiwamo ambazo hazijasajiliwa na mamlaka," alisema mkurugenzi huyo.

Alisema TMDA inawataka wananchi kutoa ama kuwezesha taarifa kupitia namba ya bure 0800110084 au kutembelea ofisi za kanda zilizoko Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Geita, Arusha, Mbeya, Mtwara na Tabora.

# GGML yatoa mamilioni kukabili maambukizi VVU

Na Mwandishi Wetu

KATIKA kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali kukabiliana na maambukizi ya Virus vya Ukimwi (VVU), Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imetoa mchango wa Sh. milioni 17 kufanikisha mbio za nyika (ATF Marathon).

Mbio hizo zilizofanyika mkoani Morogoro ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani yanayofanyika mkoani humo kitaifa Desemba Mosi mwaka huu.

Akizungumzia ushiriki wa GGML katika mbio hizo za ATF Marathon zilizofanyika Morogoro Jumapili iliyopita, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa GGML, Stephen Mhando, alisema mchango huo ni moja ya jitihada za kampuni hiyo katika kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi juu ya ugonjwa huo na kuutokomeza ifikapo mwaka 2030.

"Ufadhili huu wa GGML unathibitisha dhamira ya dhati ya kampuni yetu kudumisha uendelevu kwa watu wote. Tunalenga kuhakikisha kuwa jamii inayozunguka shughuli za mgodi wetu na hata walio nje ya Geita wanafaidika kuwapo kampuni hii.

"Fedha hizi tunaamini zitagusa moja kwa moja maisha ya watu wanaoishi na VVU, Geita ikiwa moja ya mikoa yenye idadi kubwa ya wachimbaji madini ikiwamo wasio na VVU pamoja na wenye VVU.

"Kwetu sisi GGML ni vigumu kukwepa jukumu kama hilo la kuwajali watu wa aina hii na kuwawezesha kwa namna mbalimbali," alisema.

Awali akizungumza katika hafla ya kuwapokea washiriki wa mbio hizo zilizofanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Morogoro iliyoko Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Wilson Charles, alipongeza GGML na wadau wengine kwa kuunga mkono mbio hizo.

"Ninapongeza juhudi zinazochukuliwa na wadau wetu ikiwamo GGML pamoja wananchi katika ushiriki wao kwenye Mbio za hizi za Nyika zinazolenga kutunisha Mfuko wa Udhibiti wa UKIMWI (ATF) na kuunga mkono sera ya 'Tokomeza Ukimwi, Tanzania bila Ukimwi inawezekana," alisema kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa.

Alisema wananchi wanapaswa kushirikiana na serikali katika kupambana na maambukizi mapya ya VVU ambayo hupunguza kasi ya maendeleo ya Taifa.

Mshiriki wa ATF Marathon, Neema Matheo, alisema mazoezi ni muhimu kwa mwili wa mwanadamu kwa kuwa bila mazoezi mwili hupata magonjwa yasiyoambukiza kwa haraka na urahisi zaidi yakiwamo ugonjwa wa moyo na kisukari.

Katika mbio hizo, mshindi wa kwanza wa kilomita 21 alipata zawadi ya Sh. 300,000, mshindi wa pili Sh. 250,000 na wa tatu Sh 200,000, vivyo hivyo kwa upande wa washindi wa mbio za baiskeli Km 66.

Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani mwaka huu kitaifa yanafanyika Morogoro, yakiongozwa na kaulimbiu ya 'Jamii iongoze kutokomeza Ukimwi'. Mgeni rasmi wa maadhimisho hayo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

## Makandarasi sasa kupunguziwa miradi

**Na Mwandishi Wetu,** HANDENI

WIZARA ya Ujenzi, inafikiria kuacha kutoa mikataba kwa makandarasi ambao wanachukua mradi zaidi ya mmoja kwa kuwa kitendo hicho kinachangia kusuasua kwa ujenzi wa miradi na kutokukamilisha kwa wakati.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa wilaya za Handeni na Kilindi katika kijiji cha Mafleta, baada ya kupokea kero nyingi za kutokutekelezwa kwa wakati miradi ya ujenzi wa barabara katika wilaya tatu za mkoa wa Tanga.

"Nakuagiza Mtendaji Mkuu kama nilivyokueleza kule Kwamsisi, kajipange vizuri kwa hawa makandarasi ambao si wababaishaji wapewe kazi na kwa wale ambao ni wababaishaji wasipewe kazi na wekeni vizuri mifumo wakati wa kuanza miradi mipya kwenye hatua za manunuzi na mpeana taarifa kama alishawahi kuharibu kazi sehemu na akiomba asipewe," alisema Bashungwa.

Aidha mradi wa barabara ya kilomita 20 unaotoka wilayani Handeni hadi kijiji cha Mafleta wilayani Kilindi, umegharimu Sh. milioni 30.083 ambazo ni pamoja na fidia za wananchi waliopisha ujenzi huo, na ilitakiwa ukabidhiwe Juni 6, mwaka huu, lakini umeongezewa muda wa miezi sita na utakamilika Januari, 2024.

"Mkataba huu umeongezwa mara mbili kwa kuwa ilitakiwa akabidhi barabara hii mwaka jana mwezi wa sita lakini akaongezewa tena muda sasa itatakiwa aikabidhi Januari, 2024. Kutokana na hali halisi ilivyo mpaka sasa hawezi kunidanganya kwa kuwa ana uwezo wa kumaliza barabara kwa muda mfupi uliobaki.

"Najua anataka kupewa tena kipande cha kilomita 30 kupitia mfumo wa chanzo kimoja. Nakwambia Mtendaji Mkuu wa TANROADS, mlikuwa mnafikiria kumwongezea hizo kilomita 30 lakini kutokana na mradi huu, hakuna kumpa mpaka akamilishe hizi kilomita 20," alisema.

Naye Twaha Mbwego, Katibu wa Mbunge wa Kilindi, akizungumza kwa niaba ya Mbunge Omari Kibua, alisema licha ya serikali kutoa fedha nyingi katika miradi mbalimbali ya maendeleo, bado kuna kero ya barabara inataka kufuta miradi yote mizuri iliyoletwa na serikali.

# Waziri agomea kuchangia ujenzi shule

**Na Allan Isack,** LONGIDO

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, amegoma kuchangia ujenzi wa Shule ya Msingi Mundarara mpaka apate maelezo ya kina Sh. milioni 600 zilizotolewa na serikali kuu zimetumikaje katika ujenzi wa shule hiyo.

Dk. Kiruswa, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Longido mkoani Arusha, alitoa msimamo huo baada ya kutembelea shule hiyo na kujionea ujenzi wa madarasa manane, jengo la utawala, vyumba vitatu vya maabara na vyoo havijamalizika na nyumba ya mkuu wa shule haijajengwa, milango hakuna na sakafu haijawekwa huku Sh. milioni 576 zikiwa zimetumika katika ujenzi huo.

Alisema amejulishwa kuwa fedha zilizobaki katika akaunti ni Sh. milioni nane tu na ujenzi wa shule bado haujakamilika.

Katika kata zingine za jimbo hilo, fedha za serikali kuu zilizopelekwa kiasi kama hicho, kila kitu kimekamilika ikiwa ni pamoja na kuomba usajili wa shule na imekubaliwa na serikali na kwamba Januari, mwakani, wanafunzi wataanza masomo.

Naibu Waziri huyo alisema hawezi kuchangia kiasi chochote cha fedha hadi ufanyike ukaguzi maalumu wa matumizi ya fedha zote zilizotumika na apate majibu kwa kuwa kamati ya ujenzi wa shule haishirikishwi.

"Mimi sichangii fedha yoyote hapa mpaka nipate taarifa ya mkaguzi wa hesabu kujua fedha zote zilizotumika katika ujenzi wa shule hiii. Pia nipate taarifa kwa nini kamati ya ujenzi wa shule haikushirikishwa na shughuli zote zinafanywa na mkuu wa shule," alisema.

Pia alisema iwapo itabainika kuwa fedha zimeliwa hatua kali lazima zichukuliwe dhidi ya wahusika kwa kuwa serikali inatoa fedha kwa maendeleo ya wananchi lakini kuna wajanja wachache wako kwa ajili ya kujinufaisha. Aidha, akizungumzia mgodi wa madini ya ruby unaomilikiwa na kijiji na mbia mwenza Rahmu Mollel, maarufu kama Pendeza, aliwataka wahusika kuheshimu mkataba ili kuepuka maneno yasiyo na msingi.

Dk. Kiruswa alisema katika mgodi wa Kijiji, Pendeza anahisa asilimia 75 na kijiji cha Mundarara hisa asilimia 25 lakini shughuli zote za uendeshaji zinafanywa na mwekezaji huyo na madini yakitoka kila mmoja anapaswa kupata haki yake kwa mujibu wa mkataba.

Alisema madini ya ruby yanapotoka yanapaswa kuwekwa mezani ili bodi ya usimamizi wa mgodi ya kijiji ijue na kabla ya mgawo na shughuli zote zisimamiwa na maofisa wa Wizara ya Madini kabla ya serikali kuchukua kodi yake.

Pia aliwataka waendeshaji wa uchimbaji kushirikiana na bodi ya kijiji yenye wajumbe tisa katika shughuli za kila siku na uzalishaji ili madini yakitoka kuondoa malalamiko kwa baadhi ya viongozi na wananchi kwa ujumla.

Naye Diwani wa Mundarara, Alaise Mushao, alisema mwekezaji huyo hatoi ushirikiano kwa uongozi wa kijiji na amekuwa akichukua pesa za viroba kwa wananchi na anazalisha na kuuza ruby bila kushirikisha viongozi kama mkataba unavyosema .




Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga, Kanali Maulidi Surumbu (wa pili kulia), akikabidhi mfano wa funguo ya nyumba kwa Philipho Mpika (wa tatu kulia) na Mke wake, Amina Ally (wa nne kulia), wakazi wa kijiji cha Songa Kibaoni Muheza jana, ikiwa ni makabidhiano rasmi ya nyumba waliyojengewa na mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kama fidia kupisha ujenzi wa bomba la mafuta linalotoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga. Wengine katika picha ni viongozi wa EACOP pamoja na viongozi wa serikali ngazi ya wilaya na mkoa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka TRA kuongeza kasi utoaji elimu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wafanyabiashara katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wameitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuongeza utoaji wa elimu kwa mlipakodi na ufanyaji wa biashara ili kuwapo mwamko wa wafanyabiashara kulipa kodi badala ya kutumia vitisho kama wanavyofanya baadhi ya watumishi wao.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya uzinduzi wa Wiki ya Shukurani kwa Mlipakodi, Yashiva Shan, alisema asilimia 80 ya walipakodi bado hawana utayari wa kulipa kodi na badala yake hulipa kutokana na kuogopa vitisho.

Shan alisema wataalamu hao wanapofika katika biashara, hawana lugha za kuelimisha na badala yake wanatoa vitisho na wakati mwengine wanawataka kulipa fidia jambo ambalo linajenga hofu.

"Wametuambia wamefikia malengo na kuvuka hatuwezi kuwapa hongera kwa kuwa wafanyabiashara wa mkoa huu wangeweza kukusanya zaidi endapo wangekuwa lugha za uelimishaji," alisema.

Hosiana Msuya, mfanyabiashara wa vipuri vya magari, alisema licha ya wataalamu hao kutoa elimu bado haikidhi mahitaji ya wafanyabiashara.

"Yawezekana ikawa nje ya uwezo wao lakini ni wakati mwafaka serikali kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wafanyabiashara kuhusu uzalishaji, usambazaji, uuzaji wa bidhaa ili kuleta faida itakayomwezesha mtu kulipa kodi kwa hiari. Kutoa elimu kodi tu hakumsaidii mfanyabiashara," alisema Hosiana.

Akisoma risala kwa mgeni rasmi, Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, James Jilala, alisema mamlaka hiyo imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 263 kwa mwaka 2022/23 kiasi ambacho ni zaidi ya asilimia 100 na kwamba wamevuka lengo kwa Sh. bilioni 257 kwa kipindi kilichopita.

Pia alisema kwa mwaka wa fedha unaoendelea, tayari wamekusanya Sh. bilioni 71 sawa na asilimia 72 lengo likiwa kukusanya Sh. bilioni 76 kwa kipindi cha Julai hadi Oktoba, 2023.

"Jitihada hizi ni ushirikiano wa pamoja kati ya watumishi pamoja na walipakodi ila tunakabiliwa tatizo la magendo katika maeneo mbalimbali yakiwamo Chekereni na Kahe kwa kuwa kuna hali inayosababisha upotevu wa mapato. Tuna mikakati kwa kushirikiana na taasisi za kiserikali za kuhakikisha tatizo hilo linakomeshwa,"alisema Meneja.

Naye mgeni rasmi katika wiki hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori, alisema agenda ya kuongeza mapato ni la lazima na ameitaka mamlaka husika kuongeza hali ya upatikanaji wa magari ya doria ili kudhibiti hali hiyo.



# Mpango elimu jumuishi sasa kwa vitendo

**Na Halima Ikunji,** TABORA

SERIKALI imesema itaendelea kutekeleza kwa vitendo mpango wa elimu jumuishi kwa kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimiundombinu ili kuweka usawa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na wasiyo na mahitaji maalum katika utolewaji elimu.

Kauli hiyo ya serikali ilitolewa juzi mkoani hapa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, katika mahafali ya tisa ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo (AMUCTA).

Prof. Mkenda alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kila mtoto anapata haki sawa ya elimu katika ngazi zote za masomo bila kujali hali yake ya kifamilia na kimaumbile.

Alisema ushirikishwaji katika elimu kwa watu wote si jambo la hiari bali ni haki ya msingi ya binaadamu, hivyo ni lazima kila mtu bila kujali maumbile yake apatiwe elimu bora bila ubaguzi wa aina yoyote lengo likiwa ni kuhakikisha wanatimiza malengo na ndoto zao.

“Katika kudhihirisha hili, serikali imetoa vifaa saidizi vya kidigitali kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaosoma elimu ya awali,msingina sekondarivyenye thamani ya Sh. bilioni 3.5,” alisema.

Pia alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa vifaa vya kidigitali vyenye thamani ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya wanafunzi walioko vyuo vikuu vinavyopokea wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Vifaa hivyo ni bajaji 47, komputa mpakato 172, vishikwambi 72 na vifaa vya usikivu 250.

Mwazilishi wa Chuo Kikuu hichio kishiriki hicho, Askofu Mkuu Mstaafu Paul Ruzoka, aliipongeza serikali kwa jitihada zake na kuruhusu chuo hicho kutoa elimu jumuishi na kuwasaidia wenye ulemavu kupata haki ya kielimu.

“Licha ya uhaba wa walimu uliopo chuoni hapa tumefanikiwa kupata wahitimu wa ualimu 864 na mwaka huu tumetoa wahitimu ambao ni walimu wa elimu maalum 312,” alisema Askofu Mkuu Ruzoka.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof Padri Juvenalis AsanteMungu, alisema chuo kitaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu katika kutekeleza mpango wa elimu jumuishi unaolenga kuwaweka pamoja wanafunzi wenye ulemavu na wale wasio na ulemavu ili kuleta usawa kwenye sekta ya elimu kwa kuondoa unyanyapaa kwa watoto wenye ulemavu.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, akizungumza katika uzinduzi wa utoaji kinga tiba ya kichocho na minyoo kwa wanafunzi wa miaka mitano hadi 14 wa Shule ya Msingi Nyakato katika Manispaa ya Musoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanafunzi afa maji akitafuta senene

**Na Waandishi Wetu**

ANNETH Kemileme (14), mkazi wa kijiji cha Kibale, kata ya Bwendangabo, wilayani Bukoba, amefariki dunia baada ya kuzama majini katika Mto Kyambu wakati akitafuta senene baada ya kuruhusiwa kutoka shuleni katika masomo ya kujiandaa kujiunga na kidato cha kwanza.

Baba mzazi wa binti huyo, Godwin Kemileme, alisema walipokea taarifa ya kuzama kwa binti yake juzi majira ya saa 10:jioni kutoka kwa rafiki yake ambaye walitoka wote masomoni na kuanza shughuli za kumtafuta katika mto huo.

Ofisa Habari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kagera, Shabani Mussa, akizungumza katika eneo la tukio, alisema juhudi za kuopoa mwili wa binti huyo bado zinaendelea baada ya kuupata mwili huo kwenye maji yanayotembea kisha kuwaponyoka na kuzama tena.

Katika hatua nyingine, mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Bulyanhulu, Msalala wilayani Kahama, Shinyanga, Neema Mpiga (14) anadaiwa kuroka majira ya saa 6:00 usiku na kupotea kwa zaidi ya miezi miwili sasa.

Kaka wa mwanafunzi huyo, Paul Mpiga, alisema binti huyo alipotea tangu Septemba, mwaka huu, baada ya kuondoka nyumbani hapo na kumwacha kitandani mtoto aliyekuwa amelala naye.

Alisema siku ya tukio, yeye hakuwa nyumbani lakini alipewa maelezo na mke wake kuwa waligundua kutokuwapo kwake baada ya kusikia mtoto wa miaka mitatu aliyekuwa amelala naye akilia na baada ya kwenda kumwangalia walimkuta peke yake.

Mpiga alisema tayari wametoa taarifa kwa uongozi wa kijiji pamoja na jeshi la polisi na wamepewa namba ya taarifa ya polisi yenye namba RB/1777/2023 na bado wanaendelea na jitihada za kumtafuta kwa kuwa wakati anatoroka hakukuwa na ugomvi wowote baina yao.

“Kesi za kutoroka kwa mabinti zimekuwa zikiripotiwa mara kwa mara. Ndani ya mwezi mmoja tunakuwa na kesi mbili au tatu wengine wanapatikana na wengine hawapatikani lakini tunaendelea kushirikiana kumtafuta huyu ili aendelee na masomo yake,” alisema Abasi Petro, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mkolani

Mkuu wa Shule ya Sekondari hiyo, John Masasi, alisema kweli binti huyo ni mwanafunzi wa shule hiyo hajulikani alipo na ana miezi miwili hajatokea shuleni.

Ofisa ustawi wa jamii wilaya ya Kahama Richard Ng'ondya alisema zipo taarifa za wasichana wanao toroshwa na wengine kutoroka wenyewe hivyo jitihada zifanyike kwa kushirikiana na jamii ili kumpata msichana huyo na kuendelea kupinga vitendo vya ukatili na utoroshwaji wa wanafunzi.

**•Imeandikwa na Vitus Audax na Neema Sawaka, KAHAMA**

# CCM yawaita wapinzani kuwekeza majengo yake

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, kimewaita wapinzani kutoka vyama mbalimbali kuwekeza kibiashara katika majengo yanayomilikiwa na chama hicho huku kikitaka kuweka pembeni tofauti zao za kisiasa.

Licha ya wito huo, chama hicho kimeweka sharti kwa chama chochote kitakachohitaji kuwekeza katika majengo hayo kutokusimika bendera ya chama lengo likiwa ni kutokutunishiana misuri bali kufanya biashara na kujiingizia kipato.

Wito huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlorwa, wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika mradi wa kitegauchumi cha jengo la ghorofa mali ya chama hicho lililojengwa na mwekezaji Emmanuely Komanya kwa makubaliano maalumu.

Alisema CCM imebadilika tofauti na ilivyokuwa hapo awali na sasa kinashirikiana na vyama vya upinzani ikiwa ni pamoja na kuvipa kipaumbele kuwekeza katika majengo wanayomiliki kibiashara na siyo ofisi za vyama.

Mlolwa alisema wameanza kuibua majengo ya kibiashara sehemu mbalimbali nchini ili kukisaidia chama kuingiza mapato, kukua kiuchumi na kuondokana na kuwategemea watu binafsi na wafanyabiashara katika kukisaidia chama katika shughuli zake.

Katibu wa CCM Wilaya ya Kahama, Mary Mhoha, alisema ukamilikaji wa uwekezaji huo utaongeza mapato kwa chama kutoka Sh. milioni 10.9 kwa mwaka hadi kufikia Sh. milioni 19.2.

Alisema mradi huo utakapokamilika na kuanza kufanya kazi, unatarajiwa kuingiza mapato Sh. milioni 131.4 kwa mwaka na chama kitapata Sh. milioni 65.7 kwa mwaka, sawa na asilimia 50 ya mgawo wake wa mapato ya ubia.

Mwekezaji huyo, alisema ataendelea kubaki na asilimia 50 mapato yake ya mradi kwa ajili ya kujirejeshea gharama zake kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba. Baada ya kurejesha gharama zake chama kitamiliki jengo kwa asilimia 100 na kuwataka wengine kujitokeza kuwekeza.

Ukurasa 12



**SIKU 16 Vs UKATILI KIJINSIA**
**Rais Samia aonyesha umahiri kuinua elimu ya msichana**

Ukurasa 13



**SIKU 16 ZA KUPINGA UKATILI; Ilala inavyosifika kwa juhudi za ziada kukomesha unyanyasaji wa kijinsia**


# siasa

JUMATANO NOVEMBA 29, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


SIKU 16 VS UKATILI KIJINSIA

# Ili kuwamaliza wanyanyasaji SMZ, sasa yaja na mahakama maalum kila mkoa

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAKATI dunia inaendeleza harakati za kukomesha ukatili wa kijinsia ndani ya Siku 16 za Kupinga Ukatili, kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10, Zanzibar inawajibika pia kupunguza na kuondoa dhuluma dhidi ya wanawake na watoto.

Moja ya hatua za kujivunia ni ujio na mafanikio ya Mahakama Maalum ya Makosa ya Udhalilishaji, iliyoanzishwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Ndiyo inayosikiliza na kuhukumu kwa haraka na weledi kesi za unyanyasaji na ukandamizaji kijinsia wanawake na watoto visiwani hapa, inasema Ofisi ya Jaji Mkuu wa Zanzibar.

Pamoja na hayo serikali imetunga sheria mbalimbali za kupambana na vitendo hivyo kadhalika kuongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na ubakaji, ulawiti, kuingilia kinyume na maumbile na shambulio la aibu.

Aidha, Ofisi ya Jaji Mkuu wa Zanzibar, inasema, sheria ya mwenendo wa jinai namba 7 ya mwaka 2018 , kifungu 151(1) kinachokataza kutoa dhamana kwa mshtakiwa wa kesi za ukatili na udhalilishaji nacho ni hatua ya kulinda utu wa mama na watoto wanaonyanyaswa.

Inaongeza kuwa, pia serikali imeruhusu kuongezea hukumu ambazo mahakama za awali zimezipitisha ili kufuatilia na kuona kuwa haki inatendeka.

Hata hivyo, licha ya juhudi hizo na nyingine zilizochukuliwa na zinazoendelea bado vitendo vya udhalilishaji vipo na watoto na wanawake ndiyo waathirika zaidi.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali zinaonyesha kuwa kila mwezi matukio hayo yamekuwa yakiongezeka, mfano mwezi uliopita visa 199 vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia vimeripotiwa na waathirika ni 199 wengi wakiwa ni watoto ambao ni asilimia 78.9, wanawake 16.1 na wanaume asilimia 5.0.

Idadi hiyo ya matukio 199 ni ongezeko la asilimia 26.8 kutoka matukio 157 yaliyoripotiwa Septemba 2023, ya kubaka kwa mwezi wa Septemba yalikuwa 59, wakati Oktoba yalifikia 89, ikiwa ni ongezeko la makosa 30.

Aidha matukio ya kulawiti na kunajisi Septemba yalikuwa 15, wakati Oktoba yalikuwa 22, ya kuingiliwa kinyume na maumbile Septemba yalikuwa sita, Oktoba 13, ya kutorosha Septemba yameripotiwa 11 na Oktoba ni 10.

Kati ya matukio 199 ofisi inasema,asilimia 30.2 yamefanywa na watu wa karibu katika familia wakiwamo majirani ambao ndiyo wanaotegemewa kuongeza ulinzi kwa watoto.



Riziki Pembe Juma, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. **PICHA:MTANDAO**

**KILA MKOA**

Jaji Mkuu wa Zanzibar Khamis Ramadhan Abdallah, anasema Mahakama Kuu imejiwekea mikakati ya kupunguza tatizo la udhalilishaji au kuliondoa, anayoitaja kuwa ni pamoja na kuunda mahakama maalum kwa kila mkoa.

Pia, anasema kingine ni kuteua mahakimu maalum wa kusikiliza mashauri hayo ili yasikilizwe na kutolewa maamuzi kwa haraka na kuitaka jamii kuwa tayari kutoa ushahidi pale unapohitajika mahakamani.

"Tumefanikiwa katika hilo na kwa sasa mashauri ya udhalilishaji iwapo mashahidi watapatikana kwa wakati yanachukua wastani wa miezi sita kumalizika tangu siku ya kwanza kufikishwa mahakamani,"anasema Jaji Mkuu.

Sanjari Jaji Mkuu, anasema kutokana na mikakati mahakama iliyojiwekea imefanikiwa kuhakikisha washitakiwa wanapopatikana na hatia wanaadhabiwa kisheria.

**WENGI WANAOGOPA**

"Niseme tu kuwa ingawa tatizo hili halijaisha kabisa, lakini sasa wanajamii wengi wamekuwa na hofu ya kutenda makosa hayo kutokana na adhabu zinazotolewa,"anasema Jaji Abdullah.

Aidha, kutokana na mikakati hiyo baadhi ya maeneo udhalilishaji umepungua kwa kiasi kikubwa na takwimu za mahakama za kila siku zinaonesha kuwa mahakama za Pemba zimekuwa zikipokea mashauri machache ya udhalilishaji hivi sasa.

Anasema juhudi zinaendelea kupunguza kasi ya makosa hayo Unguja kama ilivyo Pemba.

Zaina Abdallah, Mwanasheria kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania TAMWA-Zanzibar, anasema sheria ya mtoto ya mwaka 2011, inaeleza kuwa anahitaji kutunzwa kulindwa na serikali, familia na jamii.

Lakini, anasema kuna ukinzani na sheria katika kuutambua umri wa mtoto kuwa ni chini ya miaka 18, wakati sheria nyingine zimeweka miaka 14.

Aidha, anapendekeza kuwepo shule za kurekebisha tabia kwa watoto kama ilivyotambuliwa na serikali.

Kadhalika, TAMWA inaiomba serikali kuweka kipengele maalumu katika sheria, kuhusu kufanywa ukaguzi wa makazi ya mtoto ili kujiridhisha na kuepuka kuwekwa katika mazingira magumu.

"Mapendekezo yangu kwa Wiz-

INAENDELEA UK. 14

SIKU 16 VS UKATILI KIJINSIA

# Rais Samia aonyesha uthabiti wake kumuinulia elimu msichana

## •Maelfu warejeshwa darasani ufaulu la saba wazidi kupaa

**Na Sabato Kasika**

BARAZA la Mitihani la Taifa (NECTA) linapotangaza matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka 2023, linataja kuongezeka ubora wa ufaulu wa daraja A kwa wanafunzi wasichana.

Linasema ni tofauti na mwaka jana, hatua ambayo inaonyesha kuwa wanawake wanaweza na wanapopewa nafasi wanathibitisha wana uwezo.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohammed, anasema ubora wa wanawake kwenye ufaulu unaongezeka na kufikia asilimia 80.58, tofauti na mwaka jana ambao ulikuwa ni asilimia 78.91.

Anatoa ufafanuzi kuwa ongezeko hilo linahusu daraja A kwa asilimia 0.13, wakati daraja B ufaulu umeongezeka kwa asilimia 0.96 karibu asilimia moja wakati daraja C ni asilimia 0.57.

Katika wakati huu wa kuendeleza harakati za kupinga na kutokomeza udhalilishaji na ukatili wa kijinsia wanafunzi wa kike wanafanya maajabu na kuelekea kuziba pengo la wanawake kuwa chini kielimu kuliko wanaume.

Ikumbukwe ili kufikia asilimia 50/50 kiuongozi, wanawake hawawezi kupata mafanikio bila kuongeza ujuzi na maarifa na kujizatiti kielimu na kufikia viwango vya taaluma kiubobezi.

Katika juhudi za kupata usawa wa kijinsia mabinti wanajitahidi kufanya juu chini ili kuwafikia wanafunzi wenzao wa kiume na hata kwenda mbali zaidi na hiyo inaonyesha kuwa wameanza kukataa kuwa wasindikizaji na kukataa vikwazo vinavyowarudisha nyuma kitaaluma.

Miongoni mwa hatua za kuhimiza wanafunzi wasichana kusoma ni pamoja na kuanzisha sekondari maalumu za sayansi kwa kila mkoa ambazo Rais Samia Suluhu Hassan, anazijenga.

Jithada kuewandeleza na kuwatia moyo ili wajue kuwa kwenye suala la elimu si kwa ajili ya wanafunzi wa kiume, wote wako sawa, serikali pia imewaanzishia utaratibu wa kurejea shuleni baada ya kukatisha masomo kutokana na changamoto mbalimbali zikiwamo mimba na utoro.

Katika utekelezaji wa Waraka wa Elimu namba 3 mwaka 2021 wa kuwarejesha shuleni wasichana waliokatisha masomo, umewarudisha madarasani wasichana 7,995 ambao wanaendelea na masomo kupitia mfumo rasmi na usio rasmi , hivyo serikali imefanya juhudi za kuleta usawa wa kijinsia kielimu na kuwafikia hata wanawake ambao wangeachwa nje, ni kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia..

Juhudi za kufikia usawa kwenye elimu zinaonekana pia kwenye kudahili wanafunzi wa elimu ya juu, mfano, wizara inasema



Rais Samia

> Hatua ya wanafunzi wa kike kuendelea kupata ufaulu mzuri, ni wazi dhana kwamba wasichana ni wa kuolewa, inafutika miongoni mwa jamii, na sasa inawekeza kwenye elimu kwa watoto wote bila kujali jinsi.

mwaka wa 2022/23 wanafunzi 636 waliofaulu masomo ya sayansi wa kike ni 261 ambao ni sawa na asilimia 41 ya wanafunzi, wanaounufaika na Mfuko wa Ufadhili Samia Scholarship.

Lakini pia idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika taasisi za elimu ya juu nayo inaonyesha ongezeko la wanawake mfano wanafunzi 423,025 wameingizwa vyuoni, kati ya hao wa kike ni 177,905 kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia wanafunzi 555,166 wakiwemo wa kike 249,009 kwa mwaka 2022/23, ongezeko hilo la asilimia 31 kwa mujibu wa wizara pia linaonyesha namna ambavyo wasichana wanainuka kwenye elimu.

Hatua ya wanafunzi wa kike kuendelea kupata ufaulu mzuri, ni wazi dhana kwamba wasichana ni wa kuolewa, inafutika miongoni mwa jamii, na sasa inawekeza kwenye elimu kwa watoto wote bila kujali jinsi.

Watoto wa kike wanasongwa na vikwazo vingi, katika safari yao kufikia elimu ikiwamo mimba, ndoa za utotoni au wazazi na walezi kutowasomesha.

Pamoja na kuwapo mikakati ya kuwasaidia watoto wa kike kupata elimu, hali halisi katika maeneo mengi, bado kuna vikwazo mbalimbali vinavyowazuia wasichana kupata haki hiyo.

Lakini, ambao wanabahatika kupata elimu kupata ufaulu mzuri, wanapaswa kuwa mfano wa kutumiwa katika jamii ili kupambana na vikwazo ambavyo vinachangia wengine kukosa elimu.

Ni wazi kuwa ni habari njema kwa wana harakati wanaotetea haki za watoto wa kike kufurahia kwa jinsi ambavyo wamepandisha ufaulu na kupita wa mwaka jana. Kinachotakiwa ni wao kuongeza juhudi ili ikiwezekana, wawe vinara kwa kuonyesha ufaulu zaidi kwenye viwango mbalimbali.

Juhudi za serikali, walimu, jamii na wazazi pamoja na walezi , wadau wa sekta za umma na binafsi wana wajibu wa kuwatia moyo wasichana na kuwahimiza kupenda elimu na hasa kwenye masomo ya sayansi.

Njia hiyo inaweza kusaidia katika kuimarisha mchango wa utafiti na ubunifu wa kisayansi wenye tija kwa ustawi wa uchumi kwa maisha ya kizazi cha leo na kesho kupitia wanafunzi wa jinsi zote.

Kumekuwapo na juhudi za kuwahamasisha wanawake na wasichana kujikita zaidi kusoma masomo ya sayansi, uhandisi, hesabu, ubunifu na teknolojia, nguvu hiyo iendelee kutumika kuhamasisha elimu kwa jinsi zote ili watoto wa kike wasibaki nyuma.

Hata hivyo kuna tatizo sugu kila wakati linawaumiza wanafunzi ni mila na desturi za kuwaoza udogoni hili nalo lisifumbiwe macho.

Lakini pia juhudi za kuwasaidia wasichana kusoma na kufaulu udanganyifu katika mitihani, usifumbiwe macho.

Ikumbukwe udanganyifu huo unaweza kuwasaidia katika ngazi nyingine za elimu lakini hawatakuwa na mafanikio katika hatua kubwa na za juu kwenye maisha.



Baadhi ya wanafunzi wa Sekondari ya Jangwani Dar es Salaam, wakiwa katika moja ya shughuli maalum shuleni hapo hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

SIKU 16 ZA KUPINGA UKATILI;

# Ilala inavyosifika kwa juhudi za ziada kukomesha unyanyasaji wa kijinsia

**Na Sabato Kasika**



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Kipunguni, Rozina Soko, akizungumza katika kikao cha Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni cha kupanga mikakati ya kupambana na ukatili wa kijinsia. **PICHA: SABATO KASIKA**

MAENDELEO ni lazima kuunganisha nguvu za jamii na serikali ili kufanikisha juhudi za kuwezesha wananchi kusonga mbele na kubadilika kutoka maisha duni kwenda yaliyoimarika, anasema Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dar es Salaam, Francisca Makoye.

Anazipongeza hatua za kuamka na kutumia kila mbinu kuinua maisha ya jamii zinazofanyika nchini, akitoa mfano wa Halmashauri ya Ilala iliyo na vikundi kadhaa ambavyo vinajishughulisha na kuunganisha nguvu za wanajamii na serikali kuwezesha wananchi kujihudumia kuondoa umaskini na ukatili wa kijinsia.

Anakitaja kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni cha Kata ya Kipunguni ndani ya Halmashauri hiyo, akisema kimeimarika na kujikita kwenye shughuli za ujasiriamali na hatua hiyo inakwenda sambamba na kutatua changamoto zinazotokana na ukatili wa kijinsia kwa watoto .

Anaeleza kuwa kimewezesha jamii ya kata hiyo na za jirani za Kitunda na Kivule kufanya shughuli za kiuchumi na kuanzisha klabu za watoto ili kuwalinda na kuwaendeleza.

Anasema hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili kuelekea maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na kufafanua kuwa kituo hicho kimejenga ofisi ya kutolea msaada wa kisheria.

Fransisca anasema kimetumia Shilingi milioni 11, kupitia vyanzo vyake vya mapato, na kwamba kupitia ofisi hiyo na wanatoa msaada wa kisheria.

"Jamii inapata huduma hii kwa ukaribu zaidi. Pia kupitia Mfuko wa Ruzuku wa Mashirika ya Wanawake (WFT-T) kituo hicho kinatoa elimu ya madhara ya rushwa ya ngono katika jamii na imesaidia kupunguza vitendo hivyo," anasema.

### LENGO KUANZISHWA

Francisca anasema kituo kilianzishwa na washiriki wa semina za Jinsia Maendeleo zinazoratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kwa lengo la kupanua na kuongeza wigo wa kupinga ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia na kiuchumi.

Ukatili huo husababisha ukeketaji katika kata za Kitunda, Kivule na Kipunguni."Mbinu kuu wanayotumia ni uwezeshaji wa jamii kiuchumi, kifikra na pia kuendesha mijadala ya uelewa wa haki, na kwamba halmashauri kupitia Divisheni ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na wanajamii wa maeneo haya na wadau, walifuatilia kujua ni nini kinachochochea kuendelea kwa ukeketaji," anasema.

Anafafaanua kuwa wamegundua sababu zinazochochea ukeketaji kuwa unazigusa zaidi familia maskini na wasio na fursa ya kupata taarifa sambamba na kukosa ujasiri wa kupinga au kukataa.

"Ukeketaji unaambata na zawadi kwa wanaokeketwa na wazazi au walezi wao. Wakati wa maandalizi ya ukeketaji kuna baadhi ya watu au wanajamii kwao ni fursa ya kujipatia kipato wakiwamo wauza mbuzi, ng'ombe, waendesha bodaboda na wapishi," anasema.

Mkuu wa idara anasema, baada ya kujua sababu kuu ambazo zinachangia uendelevu wa ukeketaji, ndipo Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushrikiana na wadau wengine inaanza kutumia afua zake na kufanikisha kudhibiti vitendo hivyo.

"Jitihada hizo zimewezesha Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni kuhudumia watu wengi mfano mwaka 2014 walikuwa 19, wakati 2016 watu 46 walifikiwa, mwaka 2018 walikuwa 34, ilipofika 2020 walipungua hadi sita na mwaka jana walikuwa wanne, jumla ya waliohudumiwa ni 109," anasema.

Aidha, wapo waliofunzwa ujasiriamali kuanzia mwaka 2016 hadi 2023 kuwa ni wanawake 2,100, wanaume 510, vijana wa kike 2,700, wa kiume 300, watu wenye ulemavu wa kike 161 na wa kiume 71,ambao jumla ni 5,842.

"Mafunzo yanayotolewa ni mapishi, kilimo rahisi, jinsi ya kusimamia vikundi, saluni, utengenezaji wa urembo na makaa mbadala, lakini pia kuna klabu zilizoanzishwa za kupinga ukatili wa kijinsia ambazo kwa upande wa watoto zipo 30, vijana 30, za wazazi 30 za mabinti wenye watoto 30 jumla kuu ni 120," anasema Fransisca.

> "Ukeketaji unaambata na zawadi kwa wanaokeketwa na wazazi au walezi wao. Wakati wa maandalizi ya ukeketaji kuna baadhi ya watu au wanajamii kwao ni fursa ya kujipatia kipato wakiwamo wauza mbuzi, ng'ombe, waendesha bodaboda na wapishi," anasema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Seleman Biashagazi, anasema anafurahi serikali inapotambua shughuli zinazofanywa na kituo cha wananchi ndani ya jamii.

"Baada ya kazi kubwa ambayo tumeifanya ikiwamo kuanzisha klabu za kupinga ukatili wa kijinsia, kwa sasa wana jamii wenyewe wanakutana kujadili masuala ya ukatili huo na kuchukua hatua," anasema Bishagazi.

Anataja miongoni mwa hatua ambazo jamii inachukua kuwa ni kutoa taarifa kwa uongozi wa maeneo yao au katika vyombo vya dora wanapopata matukio ama viashiria vya matukio ya ukatili.

"Serikali kutambua na kuzielezea kazi zetu ni motisha kwetu. Nitoe wito kwa vikundi vingine, vifanye kazi vitatambuliwa tu. Vilevile niwaombe wafadhili kwamba wawekeze kwenye vikundi. Sisi tulianza bila msaada lakini sasa kazi zetu zinatambuliwa na serikali," anasema.

### KUNUSURU MTOTO

Bishagazi anasema kuna Umoja wa Mfuko wa Watoto (UWAMTO), na kwamba vikundi 32 kutoka kata za Chanika na Zingiziwa vilihamasika na kuamua kuanzisha umoja wao na kusajiliwa kwa jina hilo.

"Umoja huu umehamasika na kuwatambua watoto wenye mahitaji maalum na kuwahudumia kwa kuwanunulia mahitaji hayo kupitia mfuko wa Umoja wao," anasema.

Francisca anasema mfuko unawezeshwa kupitia asilimia 50 inayochangiwa kwa hisa za kila mwana kikundi kwa kila mwezi, na kwamba kila mmoja anawajibika kuchangia kulingana na mgawanyo wa ununuzi wa hisa, akitolea mfano kuwa kuna wana kikundi wananunua hisa ya Shilingi 200, wengine 500 na pia wapo wa 1,000.

Hisa zote zinapokusanywa kutoka kwa wana umoja 480 wanaotoka katika vikundi 32 inatolewa asilimia 50 inapelekwa kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum na asilimia 50 zinabaki katika umoja na kukopeshana kwa riba ndogo na kuendeleza shughuli za kiuchumi," anasema.

Anasema umoja umejikita katika shughuli za kiuchumi zinazowasaidia kupata kipato kwa ajili ya shughuli za umoja na utoaji wa huduma na pia kwa manufaa ya mwana umoja.

"Umoja huo umeshahudumia watoto160 kwa kuwanunulia vifaa vya shule kwa watoto 135 na bima ya afya kwa watoto 25, pia wamewaunganisha vijana balehe 29, wa kike wakiwa 22 na wa kiume saba.

Anasema pamoja na umoja huo, kuna vikundi 43 kutoka kata za Kivele na Gongolamboto ambavyo navyo vimeunda umoja wao ili kutatua changamoto za afya na elimu katika jamii yao.

"Umoja huu unaitwa Umoja wa Vikundi vya Ujasiriamali Kivule (UVUKI ambao unafanya jumla ya watu na watoto 1,125 kunufaika kupitia umoja huu na kunufaisha jamii inayowazunguka kutoka shule za msingi za Kivule, Gongo la Mboto na Majohe," anasema.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Wenyeji Mkutano COP Dubai wanavyougeuza changa la macho

## • Wanapigia chapuo uwekezaji nishati chafu

**Na Gaudensia Mngumi**

WAKATI Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mazungumzo ya Hali ya Hewa Duniani (COP 28) , ukitarajiwa kuanza kesho huko Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) unalenga kuuza mafuta yake.

UAE inaelezwa kupanga kutumia nafasi yake ya mwenyeji wa mazungumzo ya hali ya hewa kupigia chapua mikataba ya kuuza mafuta na gesi zake.

BBC inaripoti kuwa nyaraka za muhtasari wa mikutano hiyo zilizovuja zinaonyesha mipango ya kujadili mikataba ya mafuta na mataifa 15 washiriki wa mkutano huo.

Hata hivyo, timu ya UAE haikukataa kutumia mikutano ya COP28 kwa mazungumzo ya biashara, na ikasema "mikutano ya faragha ni ya faragha".

BBC inaongeza kuwa timu hiyo, aidha, inakataa kutoa maoni yake kuhusu kile kilichojadiliwa katika mikutano na kusema kazi yake imekuwa ikilenga "hatua ya maana ya hali ya hewa".

Nyaraka hizo zinazoelezwa kuwa zilipatikana kwa wanahabari wa kujitegemea katika Kituo cha Kuripoti Hali ya Hewa wanaofanya kazi pamoja na BBC , zinatayarishwa na timu ya UAE COP28 kwa ajili ya kupeleka ushawishi kwa serikali takriban 27 za kigeni kabla ya mkutano wa kilele wa COP28, utakaoanza kesho Novemba 30.

BBC inaeleza kuwa mazungumzo ambayo yalinaswa ni pamoja na mijadala ya namna China ambayo inasema ADNOC kampuni ya mafuta ya UAE, "iko tayari kutathmini kwa pamoja fursa za kimataifa za kuwekeza kwenye kuchakata gesi ya asilia ya (LNG) nchini Msumbiji, Canada na Australia.

Aidha, nyaraka hizo zilizonaswa zinasema Falme za Kiarabu zinapendekeza kwa Waziri wa Colombia kwamba ADNOC pia iko tayari kuisaidia Colombia kuendeleza rasilimali zake za mafuta.

Aidha, inasemekana kuna mazungumzo kwa nchi nyingine 13, ikiwa ni pamoja na Ujerumani na Misri, ambazo zinapendekeza kuiambia ADNOC inataka kufanya kazi na serikali zao kuendeleza miradi ya mafuta.



Moshi unaoongeza joto duniani kutoka kwenye mataifa yenye viwanda vikubwa.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, chombo kinachosimamia mikutano ya COP. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Aidha taarifa, zinaeleza kuwa UAE pia inatayarisha mazungumzo ya fursa za kibiashara kwa kampuni ya serikali ya MASDAR inayowekeza kwenye nishati mbadala kushirikiana na mataifa 20 ikiwamo Uingereza, Marekani, Ufaransa, Ujerumani, Uholanzi, Brazil,China, Saudi Arabia, Misri na Kenya.

Mwaka huu COP 28 inaandaliwa na UAE huko Dubai na inatarajiwa kuhudhuriwa na viongozi 167 wakuu duniani akiwamo Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani Papa Francis na Mfalme Charles III wa Uingereza.

Mikutano hiyo ndilo jukwaa muhimu zaidi duniani kujadili jinsi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### UKINZANI ULIPO

Wakati kukiwa na matumaini kwamba COP28 itasaidia kuandaa mikakati ya kupunguza ongezeko la joto la muda mrefu duniani hadi 1.5C, uwekezaji kwenye nishati za visukuku kama mafuta, makaa ya mawe na gesi asilia vitazidi kuongeza joto.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi ya Hali ya Hewa linasema ni muhimu kuachana na matumizi ya nishati hizo ili kuepuka athari mbaya zaidi za mabadiliko ya hali ya hewa, hata hivyo itahitajika kupunguzwa kwa kasi kwa uzalishaji wa gesi chafu.

Shirika hilo linataka punguzo la asilimia 43 za uzalishaji wa gesi hizo ni muhimu ifikapo 2030 kutoka viwango vya sasa.

Wataalamu wa hali ya hewa wanakubaliana kuwa nyuzi joto 1.5 hazipaswi kufikiwa ili kuzuia athari mbaya na zisizoweza kurekebishwa za mabadiliko ya hali ya hewa hivyo, wastani wa joto duniani haupaswi kuzidi ule wa nyakati za kabla ya ujio wa viwanda yaani chini ya nyuzi 1.5.

Kuanzia Januari hadi Septemba 2023, wastani wa halijoto ya dunia hadi sasa ni nyuzi joto 1.40 juu kuliko wastani wa kabla ya ujenzi wa viwanda mwaka 1850-1900.

Kwa mujibu wa mtandao wa'go.com' ikiwa joto litazidi zaidi ya nyuzi 1.5 ambalo linakadiriwa kufikiwa mwaka 2040 kuna uwezekano, kwa mujibu wa utafiti kuwa litasababisha uharibifu mbaya zaidi duniani.

Mtandao wa 'Nature Journal', unaeleza kuwa ongezeko la joto zaidi ya nyuzi 1.5 athari zake zinaweza kujumuisha, joto kali zaidi duniani katika ukanda wa tropiki ukiongezeka kwa wastani wa zaidi ya nyuzi 3.0.

Hali itakuwa mbaya zaidi kwenye ukanda wa pwani ambako kina cha maji kitaongezeka hadi robo tatu mita au karibu mita nzima, pengine ifikapo mwaka 2100 na kwamba dunia itapoteza zaidi ya nusu ya makazi yanayofaa kwa binadamu, asilimia nane ya mimea nayo itapotea na hali kuwa mbaya zaidi kwenye ukanda wa bahari.

### WACHAFUZI WAKUU

China ni mchafuzi namba moja wa mazingira duniani akichangia asilimia 30 ya hewa ukaa. Licha ya kuwa na watu wengi zaidi duniani ina soko kubwa la kuuza bidhaa nje, hata hivyo uzalishaji wa vitu hivyo umekua lakini umekuwa hatari kubwa kwa sayari hii au dunia.

Pamoja na China, yenye kuzalisha zaidi ya tani milioni 10,065 za karboni wengine ni Marekani tani milioni 5,416 , India inayotoa tani milioni 2,654, Urusi milioni 1,711, Japan tani milioni 1,162 na Ujerumani tani milioni 759.

Aidha Iran inatoa tani milioni 720, Korea Kusini, tani milioni 659 na Saudi Arabia, tani milioni 621 na mwisho ni Indonesia yenye tani milioni 615, kwa mujibu wa mtandao wa Climate Trade.

Ikumbukwe siyo nchi zote zinazochafua hali ya hewa ndiyo maana COP inawataka wachafuzi wakubwa zaidi kuchukua hatua ili kupunguza utoaji wa kaboni, lakini pia kurekebisha kiwango chao cha kaboni kwa kusaidia miradi ya mazingira kote duniani.

## ILI KUWAMALIZA WANYANYASAJI SMZ, SASA YAJA NA MAHAKAMA MAALUM KILA MKOA

INATOKA UK. 11

ara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kutengeneza muongozo maalumu wa mafunzo ya ziada ili kuwawekea mazingira mazuri ya ulinzi watoto wanapokuwa katika masomo kwa muda wote," anasema.

JAMII YAFUNGUKA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Abeda Rashid, anasema juhudi zaidi zinahitajika kuwasimamia watoto dhidi ya udhalilishaji.

Anasema mtoto anayefanyiwa udhalilishaji na ukatili anahitaji kupatiwa elimu ya kisaikolojia kwa sababu vitendo hivyo huwaathiri kiakili na kuwapa msongo wa mawazo.

Waziri wa wizara hiyo Riziki Pembe Juma, anasema kuongezeka kwa takwimu za vitendo vya udhalilishaji zinazoripotiwa kuna viashiria viwili mosi, jamii kuhamasika kuripoti kwa sababu miaka ya nyuma matukio hayo yalifichwa.

Aidha, anasema miaka ya nyuma hakukuwa na uthubutu wa kumripoti baba mzazi aliyemfanyia udhalilishaji mwanae.

'Lakini, sasa jamii imehamasika na kuelewa dhana ya udhalilishaji na hatua za kuchukua.

"Miaka ya nyuma matendo haya yalifanyika ndani ya nyumba zetu lakini nani anathubutu kuripoti, hakuna aliyethubutu kusema mume wangu anamdhalilisha mwananggu hakukuwa na ujasiri huo.

"Ni kwa sababu wanawake waliogopa talaka na aibu katika jamii lakini kwa sasa wapo kinamama wanaosimama na kusema mume wangu na mzazi wa mtoto alimfanyia udhalilishaji binti yangu au kijana wangu,"anasema.

Waziri Riziki anasema hayo ni miongoni mwa mafanikio ya kwamba jamii imehamasika kufunguka na kuwa na uelewa wa dhana ya udhalilishaji kwa sababu baadhi ya watu walidhani kuwa kudhalilishwa mtoto ni kubaka na kulawitiwa wakati kuna wanaokumbana na matukio mabaya zaidi na kupoteza maisha.

Anasema kuadhimisha siku 16 kupinga ukatili kunafanikisha kuhamasisha jamii kuzungumza na kuchukua hatua kuripoti matukio ya udhalilishaji na serikali inaendelea kusimamia sheria.

Kadhalika, anasema ukilinganisha na miaka 10 nyuma na sasa takwimu zipo juu za matukio hayo lakini vitendo bado vinaendelea katika jamii na kutaka mabadiliko.

Chimbuko la siku hizo 16 za kupinga ukatili na udhalilishaji linatokana na mkutano wa wanaharakati dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia uliofanyika Mjini Bogota Colombia Amerika ya 1981.

Ikiwa ni kumbukumbu ya mauaji ya wanaharakati wanne yaliofanywa Jamuhuri ya Domica Amerika ya Kati Novemba 25 mwaka 1960.

Baada ya UN kuridhia na kutangaza siku 16 za harakati za kupinga ukatili na udhalilishaji wa kijinsia duniani, Zanzibar ilianza kuadhimisha kwa mara ya kwanza 2011.



## UWT yabeba ajenda ya kijinsia ujenzi shule mpya za sekondari

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

MAKAMU Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Zainabu Shomari, amesema serikali itaendelea kuwekeza kwenye kuboresha miundombinu ya shule mpya za mikoa kwa ajili ya wasichana ili kuongeza usawa wa kijinsia katika kada mbalimbali nchini.

Amesema mkakati huo utasaidia kuandaa mazingira mazuri ya kujifunza na kuongeza idadi ya wataalamu wa jinsia ya kike katika kada mbalimbali nchini na kuleta usawa wa kijinsia.

Zainabu aliyasema hayo juzi wilayani hapa alipokagua ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya wasichana Mkoa wa Dodoma unaogharimu Sh. bilioni tatu katika Kata ya Manchali wilayani Chamwino.

Alisema dhamira ya serikali ni kuweka mazingira mazuri kwa watoto wa kike kujifunza ili kuongeza usawa wa kijinsia katika kada mbalimbali nchini.

Alisema shule hiyo itakapokamilika itasaidia wasichana wengi ambao watapata nafasi ya kusoma katika shule hiyo maalum ili taifa lipate wataalamu katika fani mbalimbali nchini ikiwamo wahandisi na madaktari.

Zainabu alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ya shule ya sekondari ya wasichana zinazotarajiwa kuongeza idadi na ari ya wanafunzi wa kike kupata elimu bora na kupunguza pengo la idadi ya wataalamu wanawake katika kada mbalimbali nchini.

Aliwahimiza wanafunzi kuzingatia maadili kwa kuwaheshimu walimu na kusoma kwa bidii kwa kuwa wao ndio tegemeo la taifa la kesho.

Mkurungezi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Chamwino, Dk. Semistatus Mashimba, akijibu kero za wananchi kuhusu kujengewa Kituo cha Afya Chalinze na kuongezewa madarasa katika Shule ya Msingi Chiburunge, alisema kwa kushirikiana na mbunge tayari wameshaanza utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu hiyo.

Uongozi wa UWT Taifa uko katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na umefanya mikutano ya hadhara 20.

Makamu Mwenyekiti UWT na timu yake wamekagua ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya wasichana ya mkoa, Zahanati ya Manchali na ujenzi wa mabweni matatu.

Miradi mingine iliyokaguliwa ni vyumba vinane vya madarasa na matundu 13 ya vyoo vya wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Chilonwa sambamba na kugawa kadi za wanachama wapya 100 wa CCM.

# TMDA yavisaka viwanda vinavyozalisha dawa feki

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Adamu Fimbo, amesema wataendelea kuvisaka viwanda vinavyojihusisha na utengenezaji wa dawa bandia nchini.

Pia amesema kuwapo dawa hizo kumesababisha usugu wa magonjwa mengi nchini kutokana na kutokuwa na tiba inayotakiwa kutibiwa kwa wagonjwa.

Fimbo aliyasema juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mkutano mkuu wa mwaka wa wafamasia uliofanyika jijini.

Alisema mamlaka hiyo itahakikisha viwanda hivyo vinasakwa na kuwahamasisha kuzalisha dawa zilizothibitishwa kwa matumizi ya wanadamu.

Mkurugenzi huyo pia aliwataka wafamasia kufanya kazi zao kwa weledi na kuzingatia sheria na kanuni kwa kuwa taaluma zao zinagusa uhai na maisha ya wanadamu.

"Wafamasia ni taaluma ambayo imesomewa, hivyo niwatake waliosomea wazingatie sheria na kanuni kwa kuwa taaluma yao inagusa maisha ya watu.

"Wafamasia ni wabobezi katika sekta ya dawa, hivyo mnatakiwa kuwa makini hata katika utoaji dawa na kwa kufanya hivyo, mtajiepusha kunyooshewa vidole kwa kisingizio cha kutoa dawa zilizopitwa na muda wa matumizi," aliagiza.

Pia aliwataka wafamasia ambao wanauza dawa kwenye maduka, kuwaelimisha watu umuhimu wa kumaliza dozi wanazopewa ili kujiepusha na madhara yanayoweza kujitokeza kwa kutomaliza dozi.

"Na kwa watengenezaji dawa viwandani wajiepushe pia utegenezaji dawa feki kwa kuwa wakifanya hivyo, wataangamiza maisha ya Watanzania walio wengi ambao wamekuwa wanapatiwa huduma za dawa bila kuangalia kama zinafaa kwa matumizi ya wanadamu," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alisema mamlaka hiyo itaendelea kudhibiti wanaoingiza dawa feki kwa kupitia njia za panya. Uingizaji huo umekuwa unasababisha vimelea vya magonjwa kuwa sugu kutokana na dawa hizo kutokuwa na ubora.

"Niwaombe wauzaji dawa kwenye maduka kushirikiana na mamlaka pale wanapoona na kusikia kuna udaganyifu wa uingizaji dawa ambao unaweza kuathiri miili ya watu," alisema.

Mfamasia Abel Yelelo kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba aliwataka wananchi kuacha tabia ya kununua dawa kiholela bila kuwa na cheti kutoka kwa daktari na kwa kufanya hivyo wataongeza usugu wa magonjwa kwa upande wa vimelea.

Vilevile, aliwataka watu kuzingatia maelekezo yanayotolewa na madaktari na wataalamu wa afya na wasipofanya hivyo watasababisha kupatiwa dawa zisizostahili kutokana na ugonjwa wanaougua.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph (kulia), kuhusu uchimbaji wa visima vipya katika eneo la Nzuguni, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Alhaj Jabir Shekimweri. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DUWASA yapata mwarobaini kuukabili upungufu wa maji

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKURUNGENZI Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), Aron Joseph, amesema kutokana na jitihada wanazofanya kupunguza makali ya mgawo wa maji jijini Dodoma, ifikapo mwaka 2024 upungufu wa huduma hiyo utakuwa chini ya asilimia 20.

Joseph alibainisha hayo jana jijini wakati akitoa taarifa yake kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alipotembelea Mradi wa Maji wa Nzuguni jijini.

Alisema tatizo la maji kwa Jiji la Dodoma litakuwa limepungua ifikapo mwakani kutokana na mradi huo wa Nzuguni kutarajiwa kutoa maji kwa zaidi ya asilimia 11 ya mahitaji ya jiji.

Mkurugenzi huyo alisema kwa sasa DUWASA inazalisha maji lita milioni 67.8 na mahitaji kwa jiji hilo kwa siku ni lita za ujazo milioni 133, hivyo upungufu ni lita milioni 66.7 kwa siku.

Vilevile, alisema mradi huo umefikia asilimia 99.6 na matege-meo ni kuwa kufikia mwishoni mwa mwezi ujao, makandarasi wanaotekeleza mradi huo watakuwa wamekamilisha kazi za uchimbaji visima na kujenga mtandao wa kusambaza maji.

Pia alisema katika mradi huo wanachimba visima vitano katika eneo hilo na majaribio ya awali yaliyofanyika mwezi huu, yameonesha kuwa maji hayo yanaweza kuwafikia wananchi wakati wowote.

Alisema wameanzisha uchimbaji maji kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya visima virefu vinavyokwenda chini hadi mita 300 na vitumia njia ya kompyuta kuendesha uzalishaji wa kila siku.

Aliongeza kuwa mradi huo utakapokamilika, utatoa huduma kwa wakazi wanaoishi jijini maeneo ya Nzuguni, Mahomanyika, Ilazo, Swaswa, Kisasa na Ipigala.

Alisema DUWASA imejenga matangi ya kisasa ya kuhifadhi maji kwenye mradi huo. Tangi la kwanza lina uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni tatu na lingine linahifadhi lita 500,000.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliwashukuru DUWASA kwa jitihada hizo za kuhakikisha wanawapatia maji ya kutosha wakazi wa mkoa huo.

Aliwataka wananchi kutumia fursa hiyo ya ongezeko hilo la upatikanaji maji kuboresha mazingira kwa kupanda miti kwenye maeneo yao.

Alisema mkakati wa mkoa huo katika utunzaji mazingira ni kuhakikisha kila mwananchi anapanda miti mitano kwenye eneo lake na kila mwanafunzi anapanda mti wake kwenye shule anayosoma.



HABARI MBEYA

# Asilimia 77 wanaoishi vijijini wafikiwa huduma ya majisafi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya asilimia 77 ya wananchi wanaoishi vijijini wamefikiwa na huduma ya majisafi kutokana na serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya huduma hiyo huku lengo likiwa ni kufikisha asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi alibainisha hayo juzi jijini Mbeya alipofungua kongamano la siku tatu la Chama cha Hiyari cha Mamlaka za Maji nchini (ATAWAS).

Alisema Tanzania ina jumla ya vijiji 12,308, lakini vilivyounganishwa huduma hiyo ni 9,370 na kwamba mikakati inaendelea kuhakikisha vijiji vyote vilivyobaki vinafikiwa na huduma hiyo.

Alisema Wizara ya Maji inatekeleza miradi mbalimbali ya maji kila mwaka ili kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa na huduma hiyo ikiwa ni sehemu ya uboreshaji maisha ya wananchi wote.

Naibu Waziri alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha inamtua mama ndoo ya maji kichwani kwa kutekeleza miradi ya maji ya vyanzo mbalimbali.

"Kuna baadhi ya maeneo yenye vyanzo vizuri vya maji ya mito, tunatumia vyanzo hivyo kujenga miradi ya maji na kuna baadhi ya maeneo tunachimba visima lakini lengo kuu ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma," alisema.

Naibu Waziri alisema maeneo mengi ya mijini tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji si kubwa kama ilivyo kwa maeneo ya vijijini na ndio sababu wamewekeza nguvu huko ili kuwe na msawazo.

Mwenyekiti wa Bodi ya ATAWAS, Geofrey Hilly, alisema lengo la kongamano hilo ni kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kwenye utekelezaji miradi ya maji kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi kwenye utekelezaji miradi ya maji utasaidia taifa kufikia malengo mbalimbali ya taifa.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa mataifa ambayo yameridhia mikataba mbalimbali ya Bara la Afrika na ya Dunia na hivyo alisisitiza ushirikiano huo utasaidia kutekeleza mikataba hiyo kwa ufanisi.

Baadhi ya wadau wa usambazaji wa maji nchini walioshiriki kongamano Iilo, walishauri serikali kuanza utekelezaji sera ya ushirikishaji sekta binafsi kwenye sekta ya maji.

Mmoja wa wadau hao, Ghamina Charles alisema ili kufikia malengo ya serikali, ni lazima kuwapo mafunzo ya mara kwa mara kwa wadau ili kuwajengea uwezo wa namna ya kufikisha huduma bora kwa wananchi.




Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, ACP Mtatiro Kitinkwi, akizungumza wakati wa uzinduzi wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia na watoto wa Jeshi la Polisi mkoa huo katika viwanja vya Kituo cha Polisi cha Mango Garden Dar es Salaam jana kwa udhamini wa kampuni ya Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waagizwa kutenga maeneo ujenzi shule za mchepuo wa Kiingereza

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

KAIMU Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, ameagiza Idara ya Elimu ya Msingi na Awali wilayani mwake kutafuta maeneo mapya ya kujenga shule za msingi za mchepuo wa Kiingereza ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la watu.

Athuman Bamba alitoa agizo hilo juzi wakati Kamati ya Uendeshaji ya Halmashauri (CMT) ilipotembelea shule ya mchepuo huo ya wilayani humo (Chunya Pre & Primary English Medium School).

Alisema shule hiyo imejengwa kama mfano na imeanza kuonesha wazazi wana uhitaji wa shule za mchepuo huo kutokana na wengi kuwaandikisha watoto wao kwenye shule hiyo mpya.

Alisema shule hizo zinajengwa kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri hiyo na hivyo akasisitiza maeneo yaendelee kutafutwa ili kusogeza zaidi huduma hiyo.

"Chunya inakua kwa kasi, hivyo uhitaji wa huduma kama hii utakuwa mkubwa kuliko sasa. Ofisa Elimu Awali na Msingi jaribu kutafuta maeneo makubwa na mazuri kwa ajili ya kujenga shule za namna hii," alisema Bamba.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu, Nebart Gavu, alishauri uongozi wa shule hiyo ya mchepuo wa Kiingereza kwa kushirikiana na Ofisi ya Ofisa Elimu, kuandaa mpango unaoonesha namna sahihi ya uendeshaji.

Alishauri mpango huo uoneshe idadi kamili ya wanafunzi watakaokuwa wanahitajika ili kurahisisha ukadiriaji wa idadi ya majengo yanayokusudiwa na baadaye eneo lote lipangwe mapema ili kuepuka kuvamiwa.

**Alisema shule hizo zinajengwa kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri hiyo na hivyo akasisitiza maeneo yaendelee kutafutwa ili kusogeza zaidi huduma hiyo.**

# 185 wafanyiwa upasuaji mtoto wa jicho

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

ZAIDI ya wananchi 185 wamefanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho katika Hospitali ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe bila kuchangia gharama yoyote baada ya shirika lisilo la kiserikali la Hellen Keller International kufadhili matibabu hayo.

Wakizungumza na Nipashe katika Hospitali ya Wilaya ya Wanging'ombe ambako kunafanyika upasuaji huo, wananchi hao wamesema wameanza kuona tena baada kuishi kwa kutoona kwa miaka mingi.

"Nimepona, ninaona vizuri, ninaishukuru serikali. Nilizaliwa hivi hivi, lakini ninamshukuru Mungu leo ninaona," alisema Yusta Ndetewale,

John Pondamali alisema alikuwa na hali mbaya kiasi kwamba hata maendeleo katika familia yake yamezorota kutokana na tatizo la mtoto wa jicho.

"Nilikuwa sioni lakini kupitia huduma hii, ninawaona wote sasa. Hata Mkuu wa Wilaya ninakuona," alisema Pondamali.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Dk. Frank Chiduo, alisema mpango huo umesaidia watu wengi kupatiwa huduma ya upasuaji wa macho hususani wazee ambao hupata changamoto ya macho kutokana na umri wao.

"Tatizo hili lipo katika wilaya yetu na matatizo kama haya yanasababishwa na kuzaliwa nalo, lakini kwa ajali mbalimbali pamoja na magonjwa mengine ambayo wanayapata," alisema Dk. Chiduo.

Daktari Bingwa wa Macho kutoka Wizara ya Afya, Saada Ludovick, alisema kuna takribani watu milioni tatu wenye tatizo la macho nchini na ndio maana wamelazimika kuanza kutoa huduma hiyo kwenye kila hospitali ya rufani ya mkoa.

Meneja Mradi wa Shirika la Hellen Keller International, Athuman Tawakali, alisema mradi huo ni wa mwaka mmoja unaotarajiwa kuwafikia takribani watu 900.

"Matibabu ya mtoto wajicho kama mlivyoweza kuona leo ni siku nne tayari tumewafikia watu 185 na kama nilivyosema, tunatarajia kuwatibu watu 300 kwa sababu wagonjwa bado ni wengi sana katika jamii," alisema Tawakali.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta alitembelea kambi hiyo katika hospitali ya wilaya hiyo iliyoko Kijiji cha Ihanja, akibainisha kuwa wananchi wengi wametibiwa.

"Mtakaporudi nyumbani waambieni wengine wafike wanapotangaziwa kwa sababu wataalamu wameniambia kwamba watakuja tena. Hii si mara ya mwisho. Kwahiyo, ninyi mkawe mabalozi mkawambie wajiandae kuja kupata hii huduma," aliagiza.



## ‘Mpeni msaada mkandarasi wetu’

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi ,Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, amewataka wananchi wa wilaya ya Kusini Unguja kutoa ushirikiano kwa kampuni ya IRIS ili kukamilisha ujenzi wa barabara zilizopangwa kujengwa.

Dk. Khalid aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi na wananchi wa Makunduchi mkoani humo katika kikao kilichofanyika katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja.

Alisema wizara inaendelea na utekelezaji wa ahadi za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, juu ya ukamilishaji wa barabara za ndani .

Waziri alisema tayari serikali imekamilisha ujenzi wa barabara za wilaya ya kati Unguja na sasa inahamia wilaya ya Kusini ili kukamilisha ujenzi huo .

Alisema kwa upande wa wilaya ya Kusini Unguja, serikali imepanga kujenga barabara za Jambiani Kibigija - Jambiani Mfumbwi (kilomita tano), Muungoni Skuli – Pwani Duta ( kilomita sita), Bwejuu Viamboni – Kwa lila (km 1.9) na Kajengwa Koba – Kinandi ( kilomita sita .

Mwakilishi wa Makunduchi ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora , Haroun Ali Suleiman, aliipongeza wizara kwa kazi nzuri inayoifanya na aliwataka wananchi wa jimbo hilo kuachana na propaganda zinazotolewa na baadhi ya watu.

**Waziri alisema tayari serikali imekamilisha ujenzi wa barabara za wilaya ya kati Unguja na sasa inahamia wilaya ya Kusini ili kukamilisha ujenzi huo .**

# Mijadala yatawala Z’bar kongamano Maalim Seif

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KONGAMANO la tatu la kumbukizi ya maisha ya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, limehitimishwa baada ya kutawaliwa na mijadala mikubwa.

Miongoni mwa mijadala hiyo ni pamoja na mabadiliko ya katiba, kuendeleza aliyokuwa akiyasimamia Maalim Seif akiwamo masuala ya mariadhiano ya kisiasa, uongozi na utawala bora.

Akizungumza juzi wakati akifunga, Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Taasisi ya Maalim Seif (MSF), Nassor Ahmed Mazrui, alisema kongamano hilo limefana na limetoa mwanga wa kuzidi kuimarisha nchi na kuendeleza yale yote aliyoyaacha Maalim Seif ikiwamo umuhimu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Mazrui alisema yeye ni miongoni mwa walioshiriki katika maridhiano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, na ni njia ya kufikia demokrasia na wameingia katika serikali hiyo si kwa lengo la kugawana vyeo.

Alisema wamefanya kazi kubwa na kuzunguka nchi nzima kufahamisha umma umuhimu wa (SUK) na kuwa na katiba ambayo pamoja na mambo mengine, iliwataka wakuu wa mikoa kuwa watumishi wa umma na si wa vyama vya siasa.

Mazrui alisema SUK ya mwanzo ya miaka mitano kutoka mwaka 2010 hadi 2015 iliyoundwa na CCM na CUF, ilileta mafanikio makubwa lakini mwisho wake haikuleta sura nzuri.

Hatua hiyo, alisema ilimfanya Maalim Seif mwaka 2020 kutoa onyo na kumwambia Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwamba ACT Wazalendo imeingia katika SUK kwa nia safi kwa sababu ndiyo muundo pekee wa kujenga demokrasia ya kweli katika nchi.

“Hii GNU (SUK) ni njia sahihi ya kuweka misingi madhubuti ya demokrasia ya kweli na kumaliza matatizo yote yanayotokea katika nchi hii. Kila uchaguzi baada ya miaka mitano watu wanakufa, wanaumizwa, wanaachwa walemavu, wanabakwa. Hili lazima lifikie ukomo, hatuwezi kuliendeleza

Alisema lazima viongozi kuweka SUK kweli itakayofanya kazi kwa uaminifu na kuondoa yale yote yaliyoganda na kupinda, hivyo uongozi bora uliofanywa na Rais (mstaafu) Amani Abeid Karume na Maalim Seif kuendelezwa.

Pia alisema lazima kufanya kazi kwa pamoja, kuaminiana ili kusonga mbele na aliyeshinda katika uchaguzi kumpa serikali kuongoza na kupeana madaraka, iwe kwa njia ya amani na mapenzi na kuleta mabadiliko ya kidemokrasia Zanzibar.

“Hatukuingia katika SUK kutafuta maisha wala vyeo. Sote tulioingia alhamdulillah tunamaisha yetu. Tumeishi miaka yote bila SUK bali tumejitolea kujenga nchi yetu iwe katika mazingira mazuri ya uchaguzi ya kujenga demokrasia na kuwa na Zanzibar mpya yenye maslahi kwa wote,” alisema Mazrui ambaye pia ni Waziri wa Afya.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kongamano hilo, Balozi Ali Karume alisema wazanzibari hawana itikadi ya kuwaheshimu viongozi na Maalim Seif ni kiongozi lazima aheshimiwe kutokana na mazuri yake aliyoyafanya.

Alisema Maalim Seif alisimamia na kutengeneza vizuri katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na wala hakuwa na ubaguzi licha ya kuwa na wafuasi wengi zaidi kisiwani Pemba.

Hata hivyo, alisema ifike mahali katiba iheshimiwe na ifuatwe kwa sababu ndiyo muhimu zaidi na lazima vijana kukubali kutawaliwa na kuongozwa na wazee na wasing’ang’anie kutaka madaraka.

“Huu ni wakati wa kila mtu na sio wa vijana pekee lazima kuelekezana na vijana lazima wakubali katika kupatiwa ushauri kutoka kwa wazee,” alisema.

Awali, Kiongozi wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema wakfu wa Maalim Seif aliofanikiwa ni kuwa wa wote na akiheshimu mawazo ya wengine, hakuwa na kinyongo, hivyo ni vyema wananchi kujenga utamaduni wa kuheshimu mawazo ya kila mtu.

“Maalim Seif ni wa wote kwa maslahi ya wote lazima mzingatie hili msipozingatia hili tunamdogosha,” alisema Zitto.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, akizungumza wakati akifungua kongamano la maadhimisho ya miaka 50 ya Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), katika Chuo cha Utalii Maruhubi Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# NECTA yaadhimisha miaka 50 ya kuanzishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BARAZA la Mitihani la Taifa (NECTA) limeadhimisha miaka 50 ya kuanzishwa kwake kwa kufanya kongamano ambalo limeshirikisha wataalamu kutoka Kenya, Uganda, Tanzania Bara na wenyeji Zanzibar, kujadiliana mbinu za tathmini ambazo zinaendana na karne ya 21.

Akifungua kongamano hilo lililofanyika visiwani hapa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, alisema utafiti utakaowasilishwa katika kongamano hilo, utatoa nafasi kwa watunga sera, kutunga na kuboresha mitaala ya elimu hasa kuwapima wanafunzi katika umahiri.

Waziri Lela alisema mitaala ya Zanzibar imeboreshwa ili kumjenga mwanafunzi kuwa na ujuzi ambao utamwezesha kwenda mbele katika karne ya 21 ikiwamo kujiamini, kuwa na ustadi, uvumbuzi na kutatua matatizo.

“Mpaka serikali tumefikia uamuzi wa kuondoa mitihani ya darasa la nne, na mitihani ya kidato cha pili miaka michache ijayo ni kutokana na ripoti nyingi zinazotolewa na wataalamu hawa kutushauri kwa mtaala wa sasa ambao tunakwenda nao ili mwanafunzi ajengwe kitaalamu zaidi na kuhimili mabadiliko ya karne ya 21,” alisema.

Waziri huyo alisema serikali iko katika kufanya mabadiliko makubwa ya elimu ikiwamo kipengele cha tathmini, hivyo anaamini taarifa mbalimbali za utafiti zitakazowasilishwa, zitasaidia kuleta mageuzi katika sekta hiyo.

Pia alisema kuna utafiti ambao umefanyika Zanzibar, Dar es Salaam, Uganda, Kenya, Arusha na Mzumbe na tathimini ya kutosha inayoangaliwa ni kuelezea hali ya tathmini kwa ukanda wa Afrika Mashariki hasa kuboresha upungufu ambao uko katika tathmini zinazofanyika kila siku.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Said Ali Mohammed, alisema kongamano hilo la kitaaluma limeshirikisha wadau na wataalamu hasa katika maeneo ya kutumia teknolojia kwenye upimaji, umahiri, mitaala na usimamizi wa mitihani kwa wanafunzi.

Alisema katika miaka 50, wameshuhudia mafanikio makubwa, hivyo wanafanya mapitio ya walikotoka, walipo na wanakokwenda ili miaka 50 ijayo hasa kulingana na mabadiliko ya teknolojia na matumizi ya sayansi na teknolojia katika elimu, yanafikiwa kwa kiwango kikubwa na kuendana na mabadiliko ya sasa ya ulimwengu.

Alisema hivi sasa NECTA ina lengo la kuona wanafunzi wanapomaliza shule wanakuwa mahiri kwa kutenda na kufikiri lakini matumizi ya teknolojia yamekuwa makubwa na takwimu za watahiniwa zinaongezeka kutokana na uelewa katika jamii.

“Udahili umeongezeka sana katika miaka ya hivi karibuni na utaendelea kuongezeka. Kuanzia mwaka 2018 hadi 2023 kuna mabadiliko makubwa ya idadi ya watahiniwa, hivyo kuongezeka kwao ni njia pekee kuwekeza katika teknolojia,” alisema.

Katibu huyo alisema lengo ni kuwa na Baraza la Mitihani ambalo litawavusha na kuweka heshima ya nchi kidunia katika sekta ya elimu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**PETERNOLASCO BONIPHACE KIMARO** anatangaza kupotea kwa ofa ya kiwanja **PLT.9 BLOCK "C" KISASA B CENTER-Dodoma** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/DOD/DOD/9833/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KHADUJI SALAH-FUAD ABDUL-RAHMAN,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina **Toyota Will Vi** Yenye namba za usajili **T236CUE,** Yeyote atakaeiona na atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/270958/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LEGAN HENRY MSUNGU** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 119 DQQ. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/IRI/IRI/2808/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 202/17 YA 2019**
**ABDALLAH IBRAHIM PAZI**
**(Legal Representative of Laila Godfrey)...MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**AMINA ALLY YUSUFU....................MJIBU MAOMBI NAMBA 1**
**MARIAM ALLY YUSUFU............... MJIBU MAOMBI NAMBA 2**
**SHARIFA ALLY YUSUFU............MJIBU MAOMBI NAMBA 3**
**REHEMA ALLY YUSUFU............MJIBU MAOMBI NAMBA 4**
**IBRAHIM ALLY YUSUFU............MJIBU MAOMBI NAMBA 5**
**LAURENT MZEE SECHU.........MJIBU MAOMBI NAMBA 6**

**KWA: AMINA ALLY YUSUFU**
**SHARIFA ALLY YUSUFU**
**REHEMA ALLY YUSUFU**

Mnajulishwa kwamba shauri la maombi ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es salaam tarehe 6/12/2023 saa tatu kamili asubuhi (3:00).
Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi wenyewe au mwakilishi wenu anayetambulika kisheria basi rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wenu.
Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 17/11/2023.

C. M. MAGESA
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA GEITA**
**LILILOPO GEITA**
**MAOMBI NA.54/2023**
**FERIX MLONGO............MDAI**
**DHIDI YA**
**ESTHER MASANYIWA.................MJIBU MAOMBI**

KWA ESTHER MASANYIWA popote ulipo unafahamishwa kwamba mleta maombi tajwa hapo juu amefungua shauri la madai dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Geita lililopo Geita,maombi haya yamepangwa tarehe 06/12/2023 kwa ajili ya kutajwa/kusikilizwa.
Hivyo basi unaamriwa kufika shaurini katika ofisi za Baraza saa 3 Asubuhi wewe mwenyewe au wakili wako au mtu yeyote aliyeruhusiwa kisheria.Nakala ya madai inapatikana katika Ofisi za Baraza.
KAA UKIJUA Kwamba kushindwa kufika kwako,baraza litasikiliza shauri na kutoa hukumu/maamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya baraza hili leo tarehe 15/11/2023.

.................................................
**E.MASAO**
**MWENYEKITI**
**15/11/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba, Kituo cha Katoma, Mkoa wa Kagera.**
**Shauri la Madai/ Ndoa Na. 03/2023**
**Jina la Mdai ..................Rowland R. Makere**
**Jina la Mdaiwa............ Alice S. Wawa**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa Alice S. Wawa**
Kwa kuwa Mdai/ Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao ya Talaka, hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 15 Mwezi 12 Mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 27 Mwezi 11 Mwaka 2023.

HAKIMU
.................................
**HAKIMU**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF GEITA**
**AT GEITA**
**MISC CIVIL APPLICATION No.27 of 2023**
**STEPHANO BHOKE MATHUBE ......DECREE HOLDER**
**VERSUS**
**ABED RWEIKIZYA MUKARI ........JUDGEMENT DEBTOR**
**NOTICE OF DATE FOR EXPARTE HEARING**

**TAKE NOTICE** THAT,the above case has been fixed for Exparte hearing on The 11 day of DECEMBER 2023 at 09:00 am
YOU ARE required to appear in the court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you inted to rely in support of your case.
GIVEN under my HAND and the SEAL of the Court this 27 day of NOVEMBER ,2023.

PRINCIPAL/SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE GEITA

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
**0745 700 710.**
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

HABARI KIMATAIFA

## Mahakama yasitisha mfumo mpya Bima ya Afya

**Nairobi,** KENYA

MAHAKAMA imesitisha utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2023 hadi Februari 7, mwakani.

Jaji Chacha Mwita, alitoa agizo hilo katika kesi iliyowasilishwa na mwanaharakati Joseph Aura na Muungano wa Madaktari wa Kenya (KMPDU) pamoja na Chama cha Madaktari cha Kenya (KMA), walioorodheshwa kama wahusika.

"...Agizo linatolewa kuwazuia (Rais William Ruto, Mawaziri katika Wizara ya Afya, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Ukusanyaji Mapato, Bunge la Kitaifa na Seneti), maajenti wao na au mtu yeyote juu ya maagizo yao ya kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya ya Jamii, 2023; Sheria ya Afya ya Msingi, 2023 na Sheria ya Afya ya Kidijitali, 2023 hadi Februari 7, 2024," aliagiza Mwita.

Zaidi ya hayo, mahakama iliwapa walalamishi siku saba kuwasilisha majibu yao.

Wiki iliyopita, matabibu walikosoa Sheria ya Afya ya Kijamii, wakisema ni ukiukaji wa Makubaliano ya Pamoja ya Mwaka 2017 (CBA), kuhusu utoaji wa bima ya kina ya matibabu na mwajiri.

Katibu Mkuu wa Muungano wa Madaktari Wafamasia na Madaktari wa Meno Kenya, Davji Bhimji alidokeza kwamba, sheria hiyo ilikuwa ya kibaguzi kwa watumishi wa umma na wakenya kwa ujumla. **BBC**

**"...Agizo linatolewa kuwazuia (Rais William Ruto, Mawaziri katika Wizara ya Afya, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Ukusanyaji Mapato, Bunge la Kitaifa na Seneti), maajenti wao na au mtu yeyote juu ya maagizo yao ya kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya ya Jamii, 2023; Sheria ya Afya ya Msingi, 2023 na Sheria ya Afya ya Kidijitali, 2023 hadi Februari 7, 2024," aliagiza Mwita.**

ISRAEL DHIDI YA HAMAS:

# Wafungwa watatu Kipalestina kuachiwa kwa mateka mmoja

**Gaza City,** GAZA

WAFUNGWA 33 wa Kipalestina wameachiliwa huru na kutoka magereza ya Israel, kulingana na mashirika mbalimbali ya habari.

Vyombo vya habari vinavyohusiana na Hamas pamoja na Reuters, vilisema walioachiliwa ni watoto 30 na wanawake watatu.

Shirika la habari la AFP, lilinukuu Mamlaka ya Magereza ya Israel, ikisema wafungwa hao wameachiliwa, ingawa haikueleza ni wangapi ni watoto na wanawake.

Awali, Hamas na Qatar zote zilisema Wapalestina 33 walipaswa kuachiliwa, miongoni mwao watoto 30 na wanawake watatu.

Hatua hiyo ni sehemu ya mapatano yaliyokubaliwa na Israel na Hamas, ambayo ni pamoja na kusitisha mapigano, huku zikiongezwa siku mbili zaidi.

Ni usiku wa nne mfululizo, kundi la mateka wa Israel limebadilishwa na kundi la wafungwa wa Kipalestina chini ya mapatano ya muda kati ya Hamas na Israel. Siku ya Jumatatu wiki hii, wapatanishi wa Qatar walitangaza kuongeza muda wa siku mbili wa kusitisha mapigano, ikijumuisha jana na leo.

Ikulu ya Marekani, ilithibitisha kurefusha muda huo wa makubaliano, lakini Israel bado haijafanya hivyo.

Umoja wa Mataifa (UN), umetumia utulivu huo kama fursa na kuongeza usambazaji wa misaada ya haraka kwa raia wa Gaza, huku imeonya shehena hizo ni chache.

**Shirika la habari la AFP, lilinukuu Mamlaka ya Magereza ya Israel, ikisema wafungwa hao wameachiliwa, ingawa haikueleza ni wangapi ni watoto na wanawake.**

Wananchi wa Gaza wamekuwa wakitumia muda huo, ili kupata vifaa na kuzuru eneo zima, mara nyingi wengi wakirejea makwao na kutathmini uharibifu.

Wengine walitafuta nguo za majira ya baridi huku hali ya hewa ikibadilika baada ya mvua na upepo kuanza.

**MATEKA WAELEZEA**

Wanawake 11 wa Israel pamoja na watoto walioachiliwa na Hamas, waliingia Israel usiku wa juzi, ikiwa ni wiki saba tangu kundi la Hamas, lilipowashikilia mateka na kuwapeleka Ukanda wa Gaza.

Ilikuwa awamu ya nne ya ubadilishanaji mateka kwa wafungwa wa Kipalestina katika siku ya nne ya makubaliano ya usitishaji mapigano kati ya vikosi vya Israel na Hamas, kundi ambalo Israel na Marekani, miongoni mwa nchi nyingine zimeliorodhesha kuwa la kigaidi.

Japo pande mbili zimekubaliana kurefusha muda wa usitishaji mapambano, wachambuzi wanahofu kwamba ni suala la muda tu kabla ya vita kuanza tena.

Takriban mateka 240 walikamatwa na Hamas wakati wa shambulizi lake kusini mwa Israel Oktoba 7, mwka huu, pia takriban watu 1,200 waliuawa ndani ya Israel. Baada ya shambulizi hilo la kushtukiza, Israel ilitangaza vita dhidi ya Hamas.

Kulingana na takwimu za Wizara ya Afya ya Gaza inayodhibitiwa na Hamas, zaidi ya Wapalestina 14,500 wameuawa tangu vita vilipoanza. **BBC/DW/AL JAZEERA**



Elon Musk (kushoto) na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu (katikati), walipozuru eneo la Kibbutz, Gaza. **PICHA: BBC**

# Uganda kuikopa China Dola Mil. 150

**Kampala,** UGANDA

WIZARA ya Fedha Uganda, imetangaza mpango wa kukopa dola milioni 150 kutoka kwa Benki ya Exim ya China, ili kuendeleza miundombinu ya intaneti nchini humo.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia na Naibu Waziri wa Fedha, waliwasilisha pendekezo hilo juzi, katika Kamati ya Bunge inayoshughulikia Masuala ya Uchumi wa Taifa.

Hatua hiyo inaangazia jinsi Uganda inavyozidi kutegemea ufadhili wa China baada ya Benki ya Dunia, mojawapo ya wafadhili wake wakuu, kusitisha ufadhili wake Agosti, mwaka huu, kutokana na hatua ya kupitisha sheria tata ya kupinga mapenzi ya jinsia moja.

Awali, ilichukua mkopo wenye utata wa dola milioni 200 kutoka kwa Benki ya China, ili kupanua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Entebbe (EIA).

Mkopo huo umekosolewa na baadhi ya watu, kwamba unaweka masharti ya kinyonyaji kwa Uganda.

Uganda pia iko katika mazungumzo na wakala wa mikopo wa nje wa China, Sinosure kwa mkopo wa kusaidia kufadhili bomba la mafuta kwa dola bilioni tano, ambalo Uganda inapanga kutumia kusafirisha mafuta ghafi hadi Tanzania.

**BBC**

# KUNG FU NA WUSHU SASA SHULENI

**Na Saada Akida**

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na lile la Michezo nchini (BMT), kwa pamoja wameeleza nia yao ya kuungana na Chama cha Kung Fu na Wushu (TWA), kuhakikisha michezo hiyo inaenda shuleni kwa ajili ya kukuza na kuibua vipaji.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Mtendaji wa BASATA, Kedom Elisha, katika mafunzo ya mchezo huo, ambayo yameongozwa na Mkufunzi kutoka Chuo cha Kimataifa cha Michezo Beijing, Wu Dong.

Akizungumza na Nipashe jana, Elisha alisema BASATA na BMT wanaipongeza Serikali ya China kuhakikisha wanasimama na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kila mchezo unafika shuleni.

Alisema wanaimani na Chama cha Mchezo wa Kung Fu na Wushu kwa kufanya jambo muhimu kushirikiana na Serikali ya China kuleta mkufunzi huyo ambaye amewapa semina walimu wa mchezo huo hapa nchini.

"Lengo kubwa la chama husika na Serikali ya China kuleta mkufunzi huyo ni kutoa elimu kwa walimu wa hapa nchini ili kwenda kukuza na kuufanya huu mchezo kuwa maarufu na kupiga hatua kama ilivyokuwa kwa michezo mingine," alisema Elisha. Naye Ofisa wa BMT, Nicholas Mihayo, alisema amefurahi chama cha mchezo huo kuona umuhimu wa mchezo huo kwenda shuleni kwa walimu waliopata mafunzo haya kuyahamisha katika shule na kuufanya huu kuwa maarufu na kufanya vizuri hapa nchini.

Alisema alichokipenda ni kuona chama hicho kikitoa kipaumbele kwa watoto wa kike ambao kwa sasa wamekuwa wakifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ikiwamo soka.

"Tuna ahidi kufanya kazi kwa ushirikiana na chama hicho, kwa kuwaunga mkono katika mafanikio ikiwamo walimu hao kwenda katika shule na kufundisha mchezo huo. Pia tutawaunga mkono katika mashindano ya kimataifa ambayo wanataka kuanza.

"Nilipokea taarifa kutoka kwa chama hicho kuandaa mashindano hayo na mchakato unaendelea baada ya viongozi hao kupeleka maombi Serikali ya China kuweza kusapoti mashindano hayo," alisema Mihayo.

Mkurugenzi wa Fedha na Mipango wa Chama cha Kung Fu na Wushu, Kawina Hadji, alisema wamefanikiwa kuongeza idadi kubwa ya walimu wa mchezo huo kuliko hapo awali.

Alisema kulingana na wingi wa makocha sasa wametapakaa nchini nzima tofauti na hapo awali walikuwa wachache na sasa wingi huo unaweza kufikia kila shule kuweza kutoa elimu kwa wanafunzi na kukuza michezo hiyo.

"Tumepeleka maombi ya sapoti kwa Serikali ya China kwa ajili ya kuandaa na mashindano na likifanikiwa hilo tutaenda BASATA na BMT kwa ajili ya kushirikiana ili kufikia malengo yetu. Pia kuanzia sasa tunafikiria kupeleka baadhi ya walimu kwenda shule ya Zanaki kwa ajili ya kuwafundisha na kukuza vipaji vya vijana ambao itakuwa hazina ya kesho kwa taifa," alisema.



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Mathew Kundo (kulia), akicheza muziki wakati wa maadhimisho ya Miaka 36 ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), yaliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Gee Soseji mdhamini mpya mbio za Km 5 Kili Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDAAJI wa toleo la 22 la Mbio za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon 2024, wameitangaza Gee Soseji kama mdhamini mpya wa mbio za kujifurahisha za kilomita tano, zitakazofanyika Februari 25, mwakani.

Taarifa iliyotolewa na waandaaji wa mbio hizo Dar es Salaam jana imeeleza kuwa wamefurahi sana na wanawakaribisha Gee Soseji kwa nafasi hiyo, ikiongeza kwamba mbio hizi za kilomita tano sasa zitajulikana kama Gee Soseji 5Km Fun Run.

"Mbio za Kilomita tano ni shindano kubwa linalowavutia zaidi ya wakimbiaji 5,000, hivyo Gee Soseji watapata umaarufu na kujulikana zaidi kutokana na udhamini huu mpya na ni matumaini yetu kuwa huu utakuwa uhusiano wa muda mrefu ambao utapeleka shindano hili kwa ngazi nyingine," imesomeka sehemu ya taarifa ya Kilimanjaro Marathon.

Waandaaji pia walisihi kampuni nyingine na mashirika kuona na kutumia fursa nyingine za ufadhili zinazohusiana na tukio hili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Gee Soseji, David Minja, alisema wanaona fahari kushirikiana na Kilimanjaro Marathon, moja ya matukio makubwa ya michezo katika ukanda huu.

"Kwetu sisi, hili ni jukwaa sahihi la kutangaza bidhaa zetu, kuwa pamoja na wateja katika burudani na kuwaelimisha watu juu ya lishe bora na jinsi ya kuwa na mtindo mzuri wa maisha," alisema Minja.

Alisema timu za matangazo za Gee Soseji zitakuwa Moshi kwa takriban juma moja kabla ya mbio za masafa marefu, tukio la Kilimanjaro Marathon na kukutana na wateja katika sehemu mbalimbali kama vile kwenye baa na sehemu nyinginezo na kuhakikisha wanapata uzoefu wa kuonja Gee Soseji na kushirikishana faida za lishe bora.

"Tunakusudia pia kutumia udhaminii huu kuzindua Gee Soseji na kuhakikisha zinapatikana Moshi, Arusha, Mbeya, Mwanza na hatimaye Tanzania nzima na duniani kote," alisema.

Aliwasihi washiriki wa mbio za kilomita tano kujiandikisha kwa wingi kwa vile kwa sasa wana kitu zaidi cha kutarajia kabla, wakati na baada ya mashindano yenyewe. "Tutapeleka basi kupakia wafanyakazi na wateja kushiriki na kuburudika," aliongeza.

Wafadhili wengine ni pamoja na Kilimanjaro Premium Lager (mfadhili mkuu) na Tigo -Mfadhili wa Mbio za Km 21(Kili Tigo 21Km Half Marathon), wadhamini wa meza za maji, Simba Cement, Kilimanjaro Water na TPC Sugar. Wabia rasmi ni Kili Medair, Garda World Security, CMC Automobiles, Sal Salinero Hotel na wasambazaji rasmi - Kibo Palace Hotel na Keys Hotel.

Mbio za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon 2024, zimeandaliwa na Kilimanjaro Marathon Company Limited na kuratibiwa kitaifa na Executive Solutions Ltd.

# KVZ FC, Mafunzo vitani Ligi Kuu leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Mafunzo SC inatarajia kushuka dimbani leo kupepetana na Maafande wenzao wa KVZ FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar utakaopigwa katika Uwanja wa Mau A majira ya saa 10 alasiri.

Mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu kwa timu zote kwa kuwa KVZ FC ambayo ipo katika mbio za ubingwa imetoka kupoteza mechi yake ya mzunguko wa 12 sawa na wapinzani wao, Mafunzo SC, ambao wanapigania kubaki Ligi Kuu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Mafunzo, Abdalla Bakar, alisema licha ya kuwa katika hali mbaya ya kutopata matokeo mazuri, lakini matarajio yao ni kuona mchezo huo wanapata alama tatu.

Alisema anajua anakutana na timu ngumu na nzuri ambayo ipo katika mbio za ubingwa na itacheza kwa kutaka ushindi ili kupata alama ambazo zitarejesha ari kwa mashabiki wake, lakini na wao wamejipanga kupata mtokeo.

Alisema mipango ya wapinzani wao haina tofauti na yao, isipokuwa wao Mafunzo wanatarajia kuhakikisha wanabaki Ligi Kuu Zanzibar baada ya kuwa na mwanzo mbaya.

"Tunataka kuhakikisha tunapata alama tatu, ambazo zitatutoa tulipo na kuja juu katika msimamo wa ligi, tunaweza kupata matokeo mazuri iwapo wachezaji wetu watacheza kwa ari na hamasa kubwa bila kuangalia matokeo ya nyuma tulitokaje," alisema.

Akizungumzia kuhusu wingi wa majeruhi katika kikosi chake, alisema asilimia kubwa wachezaji wa kikosi cha kwanza wameanza kupona na huenda katika mchezo wao wa leo wakawatumia baadhi yao.

Hata hivyo, amewataka mashabiki wa timu hiyo kwenda uwanjani kuipa hamasa timu hiyo ili wachezaji waweze kuhamasika kufanya vizuri.

Mafunzo inashuka dimbani ikiwa nafasi ya 13 katika msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na alama 11, wakati wapinzani wao, KVZ SC wapo nafasi ya tatu wakiwa na alama 23 katika michezo 12 waliyocheza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WERNER AULIZIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imemuulizia mshambuliaji wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner na huenda wakamnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, Januari mwakani. **(Sky Sports Germany)**

### LUIZ AWANIWA ARSENAL

ARSENA inapanga kumnunua kiungo wa kati wa Aston Villa na Brazili, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la Januari, huku mustakabali wa kiungo wa Ghana, Thomas Partey, mwenye umri wa miaka 30, ukiwa haujulikani. **(ESPN)**

### JUVE YAMTATHMINI PARTEY

KLABU ya Juventus inatathmini uwezekano wa kumnunua Thomas Partey, na huenda wakasaidia kufadhili ofa ya Arsenal kumnunua Douglas Luiz. **(Mirror)**

### CITY, LIVER VITANI

KLABU za Manchester City na Liverpool pia zinamtaka Douglas Luiz na wanatazamiwa kushindana na Arsenal kuwania saini yake. **(90 min)**

### SILVA KUUZWA

WACHEZAJI wawili ambao wanaweza kuondoka Chelsea ni beki wa Brazil, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 39, ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao na mlinzi wa England, Trevoh Chalobah, 24. **(Standard)**

### GUEHI ALENGWA UNITED

KLABU ya Manchester United imemfanya mlinzi wa safu ya kati wa Crystal Palace na England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 23, kuwa lengo lao kuelekea uhamisho wa Januari. **(Football Insider)**

### CAMARDA AIVUTIA ARSENAL

MANCHESTER City na Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa na mshambuliaji wa AC Milan na Italia, Francesco Camarda, 15. **(Tuttosport)**

### GIMENEZ LULU SPURS

Tottenham Hotspur na Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazomtaka mshambuliaji wa Feyenoord raia wa Mexico, Santiago Gimenez, 22. **(L'Equipe)**

### GREENWOOD AFUATILIWA EPL

WASAKA vipaji wa klabu kadhaa za Ligi Kuu England wamekuwa wakifuatilia uchezaji wa mshambuliaji wa England, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22 huko Getafe. **(AS)**

### EKITIKE AWANIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inaweza kumnunua kwa mkopo mshambuliaji wa Paris St-Germain, Hugo Ekitike mwenye umri wa miaka 21, katika dirisha la Januari. **(Caught offside)**

### PANDURO ATAKIWA CITY

KLABU za Manchester City na Arsenal zimewatuma wasaka vipaji wao kumtazama kiungo wa FC Copenhagen raia wa Denmark, Tristan Aldcroft Panduro, 15. **(Mail)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AMSHAWISHI REFA KUPINDUA PENALTI

**Aliungana na wachezaji wa Persepolis kupinga kuzawadiwa tuta baada ya...**

**RIYADH, Saudi Arabia**

UAMINIFU wa Cristiano Ronaldo ulisaidia kubatilishwa kwa mkwaju wa penalti aliyopewa wakati timu yake ya Al-Nassr iliyokuwa na wachezaji 10 ikitoka sare na Persepolis ya Iran kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Asia, Jumatatu.

Ronaldo alidondoka kwenye eneo la hatari katika dakika za mwanzo na mwamuzi akatoa maamuzi kuwa amechezea madhambi na kumzawadia penalti, lakini Ronaldo aliungana na wachezaji wa Persepolis kuipinga penalti hiyo.

Na baada ya mwamuzi Ma Ning kujiridhisha kwa kufuatilia, alibatilisha uamuzi wake.

Beki wa Al-Nassr, Ali Lajimi, alitolewa kwa kadi nyekundu katika kipindi cha pili kwa kumchezea vibaya Milad Sarlak.

Sare hiyo inaifanya Al Nassr kufuzu kwa hatua ya mtoano kwa kuwa mshindi wa Kundi E huku ikiwa imesalia mechi moja kuchezwa.

Timu hiyo kutoka mji wa Riyadh, iliingia kwenye mchezo huo ikiwa imeshinda michezo 18 kati ya 19 ya awali katika mashindano yote.

Katika kundi hilo hilo, Al-Duhail ya Qatar ilipata ushindi wake wa kwanza baada ya kuifunga Istiklol ya Tajikistan mabao 2-0. Mshambuliaji mahiri wa Kenya, Michael Olunga alifunga mabao yote mawili.

Mapema katika Kundi C, Kocha wa Argentina, Marcelo Gallardo, alipata ushindi wake wa kwanza tangu kuteuliwa na Al-Ittihad mwezi huu baada ya mabingwa hao wa Saudi Arabia kuwalaza AGMK ya Uzbekistan mabao 2-1 na kutinga hatua ya mtoano.

Mabao mawili katika dakika nne za kipindi cha kwanza kutoka kwa mshambuliaji wa Morocco, Abderrazak Hamdallah, yaliipatia Al-Ittihad uongozi baada ya Karim Benzema kukosa nafasi ya wazi ya kufunga.

Timu ya juu kutoka kwenye kila kundi kati ya makundi 10 ya timu nne kwenye mashindano hayo, itafuzu hatua ya 16 pamoja na washindi sita waliomaliza nafasi ya pili.

# DE BRUYNE ATAJA TAREHE YA KUREJEA




**MANCHESTER, England**

KEVIN de Bruyne amethibitisha kuwa anamatumaini kurejea Manchester City mapema mwaka 2024, huku akikaribia mwisho wa kupona kwake kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji alipata tatizo baya la misuli ya paja katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na alicheza kwa dakika 49 tu mwanzoni mwa msimu huu, kabla ya kupata jeraha lingine ambalo hatimaye lilihitaji upasuaji.

Mapema mwezi huu, De Bruyne alilinganisha misuli yake ya paja na "taulo ya jikoni iliyolowa" huku akikiri ukubwa wa uharibifu uliopatikana, lakini alikiri kuwa hajui tarehe ya kurudi dimbani.

Kwa kuwa sasa amefanyiwa uchunguzi huo, De Bruyne aliiambia Sky Sports F1 alipokuwa mgeni kwenye mashindano ya Grand Prix ya Abu Dhabi yanayoisha msimu huu kwamba atarejea dimbani mapema 2024.

"Naendelea vizuri," alisema juu ya kupona kwake. "Bado tuna njia ndogo ya kwenda, lakini tutafika."

Alipoulizwa tarehe anayoweza kurejea, De Bruyne aliongeza: "Tunatumaini kuwa kuna kitu karibu baada ya mwaka mpya, ikiwa kila kitu kitaenda sawa."

City watamaliza kampeni zao za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Desemba kwa michezo dhidi ya RB Leipzig na Crvena zvezda, huku kikosi hicho cha Kocha Pep Guardiola pia kikiwa na mechi sita za Ligi Kuu England kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Tottenham Hotspur ndio wapinzani wanaofuata kwenye ratiba ya nyumbani, wakifuata Aston Villa, na De Bruyne ni wazi hataweza kuwakabili.

De Bruyne pia atakosa kampeni ya kwanza ya City Klabu Bingwa Dunia ya FIFA, ambayo inatazamiwa kuanza Desemba 19, mwaka huu kwa mechi ya nusu fainali dhidi ya Leon ya Mexico au Urawa Red Diamonds ya Japan.

Mchezo wa mchujo wa mwisho na wa mshindi wa tatu utafanyika Desemba 22, mwaka huu nchini Saudi Arabia, siku tano tu kabla ya City kurejea England kucheza na Everton.

# Wolves kumng'oa Ramsdale Arsenal

**LONDON, England**

KLABU ya Wolves inadaiwa kuwa kwenye mpango wa kuwasilisha ofa kwenda Arsenal ili kumsajili mlinda mlango wa timu hiyo na England, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 27, kwa mkopo katika dirisha lijalo.

Wolves imepanga kufanya hivyo baada ya kuona Ramsdale hapati nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Arsenal tangu kuanza kwa msimu huu ambapo Kocha Mikel Arteta amekuwa akimtumia zaidi David Raya.

Mbali ya Wolves, kulikuwa na ripoti zilizodai kwamba Bayern Munich pia inafikiria kuwasilisha ofa na kumsajili staa huyu ili akachukue nafasi ya Manuel Neuer ambaye amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara na umri ukimtupa mkono.

Ramsdale ambaye msimu uliopita alikuwa mmoja kati ya wachezaji tegemeo kwenye kikosi cha kwanza cha Arsenal, mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika mwaka 2026. Tangu kuanza kwa msimu huu amecheza mechi nane za michuano yote.



# Chelsea kutuma ofa kwa Osimhen Januari

**LONDON, England**

CHELSEA iko tayari kutoa ofa yao kwa mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen, kwenye dirisha la usajili la Januari, kwa mujibu wa 90min.

Osimhen amekuwa mshambuliaji anayelengwa na Chelsea kwa muda mrefu, lakini 'The Blues' hao walianza kutafuta shabaha nyingine msimu uliopita ilipoonekana kana kwamba mchezaji huyo wa Kimataifa wa Nigeria angesaini mkataba mpya huko Naples.

Ivan Toney, Santiago Gimenez na Lautaro Martinez, walikuwa miongoni mwa wale waliokuwa wakifuatiliwa.

Hata hivyo, masuala yameibuka katika mazungumzo ya Osimhen na Napoli na vyanzo vimeithibitishia 90min kwamba kuna uwezekano mdogo wa kukubali kuongezewa muda licha ya juhudi zinazoendelea za klabu yake.

Hilo limeipa Chelsea matumaini kwamba huenda wakamnunua Osimhen mwaka 2024 - na ingawa uhamisho wa majira ya joto unabaki kuwa matokeo yanayowezekana, na The Blues wako tayari kujaribu kutoa ofa kwa Napoli Januari.

Chelsea wanafahamu vema kwamba huenda wakahitaji kuvunja rekodi yao ya uhamisho wa kumnunua Osimhen mwenye umri wa miaka 24, ambaye bei yake inatarajiwa kuzidi pauni milioni 115 iliyotumika kumnunua Moises Caicedo kutoka Brighton & Hove Albion msimu uliopita.

Wakati Napoli wakisalia kutaka kumbakiza Osimhen, wanaweza kulazimika kusikiliza matakwa huku mshambuliaji huyo akiingia miezi 18 ya mwisho ya mkataba wake.

Chelsea pia ni miongoni mwa timu zitakazomtaka mchezaji mwenzake na Osimhen wa Napoli, Khvicha Kvaratskhelia, ambaye yuko kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba wake.

Napoli wamesisitiza kwamba hawatapoteza mali zao hizo mbili kwa mwaka mmoja, huku Osimhen akiwa na uwezekano mkubwa wa kuruhusiwa kutoka pale kwenye dimba la Diego Armando Maradona.

HABARI MICHEZO

# SIMBA, YANGA KUKINUKISHA LIGI KUU YA WANAWAKE JANUARI 3

**Na Saada Akida**

BODI ya Ligi Tanzania (TBPL), imetangaza rasmi kuanza kwa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ikitarajiwa kuanza Desemba 20, mwaka huu, huku mechi ya watani wa jadi, Simba Queens dhidi ya Yanga Princess ikipigwa Januari 3, mwakani.

Simba Queens watakuwa nyumbani kuwakaribisha Yanga Princess katika uwanja ambao bado haujawekwa wazi, lakini awali walikuwa wakitumia dimba la Benjamin Mkapa au Uhuru, Dar es Salaam, mechi ikipigwa saa 10:00 alasiri.

Desemba 20, mwaka huu, kutakuwa na mechi tatu, Bingwa Mtetezi, JKT Queens, atakuwa ugenini dhidi ya Bunda Queens, katika Uwanja wa Karume uliopo Mara huku Simba Queens ikivaana na Ceasiaa Queens, kwenye Uwanja wa TFF Centre Kigamboni.

Mechi zingine za tarehe hiyo itawakutanisha Alliance Girls dhidi ya Geita Gold Queens katika Uwanja wa Nyamagana (Mwanza) na Fountain Gate Princess wakiwakaribisha Amani Queens Dimba la Jamhuri, Desemba 21, Baobob Queens watakuwa nyumbani ikiwakaribisha Yanga Princess katika uwanja wao, jijini Dodoma.

Desemba 27, mwaka huu, Geita Gold Queens itashuka dimbani dhidi ya JKT Queens, Nyankumbu, Desemba 28, Simba Queens wakiwakaribisha Baobab Queens Uwanja wa TFF Kigamboni na Januari 2, mwakani, kutakuwa na mechi kati ya Alliance Girls dhidi ya Fountain Gate Princess, Uwanja wa Nyamagana. Siku hiyo pia Baobab Queens itaikaribisha Bunda Queens Uwanja wa Jamhuri. Ceasiaa Queens dhidi ya Geita Gold Queens (Samora) na Amani Queens ikiwakaribisha KT Queens (Ilulu).

Kabla ya mchezo huo wa ligi kupigwa, timu hizo mbili zitakutana tena msimu huu katika mchezo wa Ngao ya Jamii, Simba wakiwa wenyeji dhidi ya Yanga Princess kutafuta mshindi ambaye ataenda kucheza na mshindi wa mchezo kati ya Bingwa Mtetezi, JKT Queens dhidi ya Fountain Gate Princess, mechi zote zitachezwa Desemba 9, mwaka huu, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Simba Queens kwa sasa iko chini ya Kocha Mkuu, Juma Mgunda, akisaidiwa na Mussa Hassan Mgosi, mazoezi yakifanyika Uwanja wa Mo Arena uliopo Bunju, huku Yanga Princess ikinolewa na Fred Mbuna na wakijifua kwenye Dimba la Uhuru.




Wachezaji wa Simba wakiendelea na mazoezi katika Uwanja wa Mo Arena uliopo Bunju, Dar es Salaam, kujiandaa na mechi ya Kundi D Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, Jumamosi wiki hii. **PICHA: SIMBA**

# Mgaza awatesa Baleke, Pacome, Feisal Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Yassin Mgaza wa Dodoma Jiji FC, anaongoza kwa kufunga bao la mapema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, akiwapiku mastaa kina Pacome Zouzoua na Keneddy Musonda wote wa Yanga, Feisal Salum na Prince Dube (Azam FC) na Jean Baleke wa Simba.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Bodi ya Ligi, Mgaza hadi kufikia raundi ya 11 anaongoza kwa bao la mapema, akifunga dakika ya pili ya mchezo katika mechi kati ya timu yake na Tabora United iliochezwa Oktoba 6, mwaka huu katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

Katika mechi hiyo, Dodoma Jiji ilifungwa mabao 2-1 na wenyeji wao.

Feisal, Pacome na Musonda wanafuatia kwa mabao ya mapema, ambapo kila mmoja alifunga dakika ya tatu ya mchezo kwenye mechi tofauti ambazo timu zao zimecheza.

Agosti 16, Feisal alifunga bao dakika ya tatu katika mechi ambayo timu yake, Azam FC iliiadhibu Tabora United mabao 4-0, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam akipiga pia 'hat-trick' siku hiyo, huku Pacome akifunga bao dakika hiyo, Oktoba 4 kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya, katika mechi ambayo timu yake ilifungwa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC.

Straika Musonda, yeye alipachika bao dakika ya tatu kwenye mechi ya watani wa jadi, Novemba 6, akiiongoza timu yake kuibugiza Simba mabao 5-1.

Dube, Maguri wa Geita Gold na Baleke mabao yao waliyafunga dakika ya tano ya mchezo. Baleke akifunga Agosti 17, Simba ikiifunga Mtibwa Sugar 4-2, Dube akifanya hivyo katika mechi dhidi ya Tabora United na Maguri akifunga katika mechi ambayo Geita Gold ilicheza dhidi ya Ihefu.

## Benchikha aonya mastaa Simba

INATOKA UK. 24

mmoja mmoja na kesho, Alhamisi kuanza kazi rasmi.

"Ujio wa Benchikha vilio sasa basi, vimefika kikomo, hawa watu wamekuja kutufuta machozi, amekuja kutupatia maisha mapya ndani ya Simba.

"Suala la usajili amekabidhiwa kocha huyo baada ya kuona kikosi chake ataeleza ni wapi afanye maboresho kwa kuongezea watu, hilo linakuja baada ya kuona timu yake," alisema Meneja huyo.

## Yanga: Al Ahly wameshikilia heshima yetu

INATOKA UK. 24

ni mpinzani mkubwa, hivi karibuni anakwenda kucheza Klabu Bingwa Dunia, atakwenda kucheza na klabu kubwa barani Ulaya kama Manchester City na nyinginezo, maana yake huyu ni mpinzani sahihi kwetu na ataiheshimisha klabu yetu kama tukipata matokeo mazuri," alisema Kamwe.

Itakuwa ni mechi ya pili ya Yanga kwenye Kundi D, baada ya ile ya awali iliyopita kupokea kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya CR Belouizdad nchini Algeria na inahitaji ushindi ili irudi kwenye reli ya kuelekea hatua ya robo fainali.

Al Ahly, ikiwa nyumbani Jumamosi iliyopita nayo iliichakaza Medeama ya Ghana mabao 3-0.

Mabingwa hao watetezi, Al Ahly, wapo juu kileleni mwa msimamo wa kundi hilo kialfabeti tu, wakiwa sawa kwa kila kitu na CR Belouizdad iliyo kwenye nafasi ya pili, huku Yanga nayo ikiburuza mkia kialfabeti pia kwani iko sawa kila kitu na Medeama iliyokaa nafasi ya tatu.

Wakati huo huo, Rais wa Klabu hiyo, Injinia Hersi Said, amesema Klabu ya Yanga ni ya watu wote Bara na Visiwani, hivyo hafurahishwi na wale wanaoiita Dar es Salaam Young African, badala yake anataka iitwe Young African au Yanga.

Akizungumza mjini Zanzibar wakati akifungua Tawi la Yanga, Taveta Mjini Unguja jana, Hersi alisema kitendo cha kuiita Yanga kwa jina la Dar es Salaam Young African, kunakuwa na dhana kwamba ni ya watu wa Dar tu.

"Hii inaitwa Young African, kwa kifupi ni Yanga na siyo Dar es Salaam Young African kama inavyoitwa na baadhi ya wanachama, mashabiki, wadau wa michezo na hata vyombo vya habari.

"Nini maana yake, ni kwamba hii klabu ya kwetu wote na wala si ya watu wa Dar es Salaam tu na pia kila tawi hapa nchini lina nafasi sawa na matawi yote Tanzania," alisema.

# Michezo

Jumatano Novemba 29, 2023
Nipashe




**Ronaldo amshawishi refa kupindua penalti** UKURASA 21

**KAZINI KUNA KAZI...**




Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, akiwa na wasaidizi wake, Farid Zemiti (kocha msaidizi) na Kamal Boudjenane wa viungo, baada ya kuwasili Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana, wakitokea kwao Algeria. **PICHA: SIMBA**

# BENCHIKHA AONYA MASTAA SIMBA

## ●●●Ashikilia namba zao, aahidi mashabiki raha 'mfululu', asema yeye ni mpambanaji, hivyo...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Mualgeria Abdelhak Benchikha, ameanza kuonesha makucha yake kwa kusema hatoangalia ukubwa wa jina la mchezaji au kipenzi cha nani, zaidi ya kutaka kuona kiwango bora na kupambania klabu hiyo kufikia malengo.

Benchikha tayari amewasili huku akiambatana na wasaidizi wake wawili, Farid Zemiti ambaye atakuwa kocha msaidizi na Kamal Boudjenane wa viungo.

Kocha huyo tayari yuko nchini kuchukuwa nafasi ya Robertinho Oliveira na wenzake kuendelea kukinoa kikosi cha 'Wekundu wa Msimbazi' hao wakijiandaa na mchezo wa pili wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Benchikha amesaini mkataba wa mwaka mmoja na nusu wa kukinoa kikosi hicho kuhakikisha kinafikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa ligi ya ndani na kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha alisema malengo yao ni kufanya vizuri, hivyo lazima kila mchezaji anatakiwa kupambana na si kujiona mkubwa ndani ya timu kwa sababu lengo lake kubwa ni kuifanya timu hiyo kupata ushindi uwanjani na kutwaa mataji mbalimbali ya ligi ya ndani na kufikia malengo katika michuano ya kimataifa.

Alisema ili timu kupata mafanikio, lazima kuwapo kwa mshikamano baina ya timu, viongozi na mashabiki kuisapoti timu yao.

"Ninafuraha kuwa sehemu ya familia ya Simba, ni timu kubwa Afrika, ni furaha kuwapo sehemu ya historia ya hapa. Tupo pamoja na mashabiki wa Simba na wanatakiwa kuwa imara kuvuka katika hili na tupo tayari kuwapa kiwango bora uwanjani.

"Kuna vingi navijua, nimekuja na mikakati yake na nitapata nafasi ya kuona wachezaji wangu na kuangalia yupi ananifaa au hanifai, suala la mashindano ninaimani nitafanikiwa kufanya vizuri kwa sababu mimi ni mpambanaji," alisema Benchikha.

Aliongeza kuwa anaimani atawafurahisha mashabiki kwa kutengeneza Simba mpya na imara, kikubwa anahitaji sapoti na ushirikiano mkubwa kutoka kwao na kufanikisha kile ambacho wanakitarajia.

Kocha huyo alisema amekuja kwa malengo ya kufanikiwa kwa Klabu ya Simba kama ilivyo kwa klabu alizotoka kubwa zaidi ni ushirikiano mkubwa.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Iman Kajula, alisema wanatamatisha shauku ya mashabiki kumpata mwalimu na kwamba walipokea wasifu nyingi kutoka kwa makocha mbalimbali, lakini walikuwa na kipindi kigumu kupata kocha mzuri kama ilivyo kwa Benchikha.

"Benchikha atakuwa Simba, atamalizia msimu huu na msimu ujao, mashabiki wanatakiwa kuwa watulivu kwa sababu ni kocha mpya, viongozi tumempa uhuru wa kufanya kazi na hatuna utaratibu wa kumpangia kocha kikosi nani acheze na asicheze," alisema Kajula.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, ametamba kuwa wamepata kocha mzuri, Benchikha, ambaye yuko katika orodha ya makocha watano bora wanaowania tuzo ya kocha bora Afrika.

Alisema ni kocha mwenye uzoefu mkubwa, hivyo wanaimani ya kufikia malengo yao kwa sababu ya falsafa ya Benchikha kutaka ushindi na mafanikio katika klabu ambayo anaifundisha.

"Wakati tuko kwenye mazungumzo alituomba tumweleza mipango yetu ya sasa na ijayo, tukafanya hivyo na kukubaliana nasi na amekuja na wasaidizi wake akiwa na kocha msaidizi na viungo.

"Matarajio yetu makubwa kulingana na kocha tuliyempata, huyo kazi ataifanya kikubwa ni kumpa ushirikiano na muda. Ni kocha mwenye msimamo kweli kweli, tutampa uhuru katika kazi yake na wachezaji wamemwahidi kumpa ushirikiano mkubwa," alisema Ahmed.

Alisisitiza kuwa benchi la ufundi halitaingiliwa kwenye majukumu na maamuzi yao, na jana alitembelea kambi ya mazoezi na leo atakuwa na kibarua cha kuzungumza na mchezaji

INAENDELEA UK. 23

## Yanga: Al Ahly wameshikilia heshima yetu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema mechi ya Jumamosi dhidi ya Al Ahly imeshikilia heshima yao kwani kama ikiibuka na ushindi itapata sifa kubwa barani Afrika na pia itarudisha matumaini yao na malengo ya kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Akizungumza jana mjini Zanzibar, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema kwa sasa wapo Unguja kwa ajili ya kupata baraka kutoka kwa wazee, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kwa ajili ya mechi ya Jumamosi itakayochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Tuko Zanzibar kwa ajili ya kupata baraka, kuelekea katika mechi yetu dhidi ya Al Ahly, ni mchezo mkubwa ambao umeshikilia heshima yetu barani Afrika,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >